SportPesa
TZS. 878,152,880
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Wanasaikolojia** wafunguka chanzo kasi matukio mauaji

UKURASA 4



**WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA MABAO 100 HARAKA ZAIDI**

UKURASA 12


# Nipashe

**Jumatatu Januari 31, 2022** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580842

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Duni: Dhamana kubwa kwangu

• **Ni** baada ya kurithi mikoba ya Maalim Seif ACT, aanika atakayoanza nayo... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**
**MCHUANO UNAIBU SPIKA KITENDAWILI**
KINYANG'ANYIRO cha kumpata Spika wa Bunge kinatarajiwa kufika tamati kesho baada ya wabunge kupiga kura...

**UKURASA WA 3**
**VIONGOZI CHADEMA WALIVYOTUMBULIWA**
CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kimevunja uongozi wa...

**UKURASA WA 18**
**MWANZA YATOA SABABU KUPAA CHANJO UVIKO-19**
MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Ruta Thomas, amesema, kilichoufanya mkoa wake kuwa miongoni mwa...


## Mwanafunzi anusurika ndoa kwa mahari ya ng'ombe 14

UKURASA 4



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akitoa maelekezo kwa Katibu Mkuu (Sekta ya Ujenzi), Balozi Aisha Amour, alipokagua daraja jipya la Selander (Tanzanite), lililokamilika ujenzi wake kwa asilimia 100 na kuanza kutumika rasmi kuanzia kesho jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Rogatius Mativila. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Daraja la Selander rasmi kesho bila ya kutozwa malipo

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA: MOTO HUU HAUZIMIKI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Daraja la Selander rasmi kesho bila kutozwa malipo

**Na Gwamaka Alipipi**

DARAJA jipya la Selander lililoko jijini Dar es Salaam litaanza kutumika rasmi kesho alfajiri bila watu kulipia, baada ya ujenzi wake kukamilika kwa asilimia 100.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, jijini Dar es Salaam jana wakati akikagua Daraja jipya la Selander (Tanzanite) lenye urefu wa kilomita 1.03, upana wa mita 20.5 ambalo ujenzi wake umekamilika kwa kiwango hicho.

Prof. Mbarawa alisema ujenzi umeshakamilika kwa asilimia mia, kwamba kuanzia Februari mosi saa 12 alfajiri magari yataanza kupita rasmi.

Alisema kukamilika kwa daraja hilo kutapunguza msongamano wa foleni kwa asilimia kubwa kwa wananchi wanaofanya shughuli zao katikati ya Jiji.

"Tanzania inaanza kufunguka kiuchumi, daraja hili litakuwa mkombozi kwa wananchi wengi. Hivi sasa tunamsubiri Rais Samia Suluhu Hassan kuja kulifungua rasmi lakini magari yataanza kupita Februari mosi. Niwaombe TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania) wahakikishe wanalitunza, Watanzania wasiharibu miundombinu," alisema Prof. Mbarawa.

Aliongeza kuwa hakutakuwa na malipo yoyote kwa magari yatakayopita katika daraja hilo, kwamba vyombo vyote vya usafiri pamoja na waenda kwa miguu watapita bure.

Kadhalika, Prof. Mbarawa alielezea mkakati wa serikali wa kuanza ujenzi wa daraja katika eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam kwa kusema kuwa maandalizi yameanza, kwamba muda wowote kuanzia sasa itatangazwa zabuni ya kumpata mkandarasi.

Naye Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila, alisema kukamilika kwa Daraja la Selander kumegharimu Sh. bilioni 243, limejengwa na Kampuni ya GS Engineering ya Korea.

Alisema Daraja la Selander lina nguzo za msingi 254, vitako 16 pamoja na nguzo 16 za juu, nyaya za daraja 30 pamoja na barabara unganishi zenye urafu wa kilometa 5.2.

Katika hatua nyingine, Prof. Mbarawa amewaagiza mameneja wa TANROADS kila mkoa, kuhakikisha wanafanya ukarabati wa barabara pamoja na kuweka alama ili kupunguza matukio ya ajali ambayo yameanza kushamiri.

Pia amewataka kufanya ukarabati katika madaraja makubwa ikiwamo kuondoa mchanga ili mvua zitakaponyesha maji yaweze kupita pasipo kuleta uharibifu.

Prof. Mbarawa alisema: "Matukio ya ajali yamekuwa mengi sana, sababu ni uzembe wa madereva pamoja na ubovu wa barabara. Nawaagiza mameneja wote wa mikoa wa TANROADS kuhakikisha wanakarabati barabara zao. Pia wahakikishe madaraja yote maji yanapita, jana nimeona Daraja la Dumila maji yanapita juu ya daraja, ile hali sitaki kuiona."

# Samia kuwa mgeni rasmi Siku ya Sheria

**Na Hellen Mwango**

UONGOZI wa Mahakama ya Tanzania, umesema Rais Samia Suluhu Hassan anatarajia kuongoza sherehe za Siku ya Sheria Februari 2, Chinagali jijini Dodoma, badala ya Februari Mosi, 2022.

Hatua ya kuahirisha sherehe hizo ambazo zilikuwa zifanyike Februari mosi, imetokana na sababu zisizoweza kuzuilika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano Mahakama, Tiganya Vicente, kaulimbiu ya mwaka huu ni, 'Zama za Mapinduzi ya nne ya viwanda; Safari ya maboresho kuelekea Mahakama Mtandao.'



Wakazi wa Kata ya Kikuyu Kusini jijini Dodoma wakishiriki kufanya usafi wa mazingira kwenye maeneo yao mwishoni mwa wiki. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Duni: Dhamana kubwa kwangu

**Maulid Mmbaga na Enock Charles**

MRITHI wa Maalim Seif Shaarif Hamad katika uenyekiti wa ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji maarufu 'Babu', amesema dhamana aliyopewa ni kubwa sana.

Duni alitoa kauli hiyo, baada ya kuchaguliwa kushika wadhifa huo jana alfajiri mkoani Dar es Salaam.

Wajumbe wa chama hicho mbali na kumpa Duni dhamana hiyo, pia waliwachagua Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, na mjumbe wa Halmashauri Kuu Msafiri Mtemelwa.

Uchaguzi huo ulijumuisha wajumbe 470, waliopiga kura ni 468, kura zilizokataliwa ni nne na halali ni 464.

Nafasi ya uenyekiti ilikuwa ikiwaniwa na watu wawili ambao ni Hamadi Masoud Hamadi ambaye alishika nafasi ya pili kwa kupata kura 125 (asilimia 26.9), huku Duni akishinda kwa kupata kura 339 (asilimia 73.06).

**KAULI YA DUNI**

Baada ya kuteuliwa, aliwashukuru wajumbe wa chama hicho kwa kumpa dhamana hiyo huku akisema ni kubwa sana.

Duni alisisitiza kuwapo umoja na ushirikiano katika chama hicho, akisema kuwa wote ni wamoja na wanajenga nyumba moja.

"Dhamana hii ni kubwa sana, mara nyingi wengi hufurahi kuwa wameshinda, lakini maana yake ni unabeba si dhamana ya wana-ACT tu ila Watanzania wote wanaangalia kimetokea nini... leo nawaahidi sitawaangusha, na kutakuwa na ustahimilivu kwani ulezi niliozoea ni kwamba watu wote ni sawa," alisema Duni, mwanasiasa nguli.

"Kwa hivyo ninapowaita kwa jina la kawaida la Babu nanyi msione tabu kuniita Babu kama vile mnavyotaka," aliongeza.

Shukrani nyingine ziende kwa viongozi wa chama wa taifa, si rahisi kwa huko tulikoanza, watu wengi walisema sasa Chama cha ACT kimekwisha, lakini sasa alhamdulilahi tumevuka tena mtihani huo."

Aliongeza kuwa katika chama hicho wameendelea kuwa wamoja, huku akiwashukuru wale wote waliokuwa wakimweleza udhaifu wake akisema kuwa wamekuwa wakimsaidia kujua wapi anapatia na wapi anakosea.

Pia aliishukuru kamati ya uchaguzi kwa kutekeleza jukumu hilo, na kwamba angeshindwa asingekuwa na sababu ya kulalamika. Pia aliishukuru kamati ya uongozi kwa kuhakikisha wanasimamia suala hilo kwa weledi hadi kukamilika.

Alisema kwa sasa wanarudi kujenga chama chao, akieleza kuwa ataanza kufanya ziara za kwenda kuzungumza na wanachama katika maeneo tofauti ili kuwazindua na kujiandaa kuwa mbele kuna uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu, hivyo wajiandae.

"Uzoefu nilionao na kwa ushirikiano na viongozi wa taifa nitafanya kila liwezekanalo chama hiki kiwe ni matumaini ya Watanzania, pamoja na tabu nyingi mlizopata, lakini mumekuja kutimiza wajibu wenu," alisema Duni.

**DUNI NI NANI**

Alizaliwa Novemba 26, 1950, Zanzibar, na kupata elimu katika Shule ya Msingi Mkwajuni mwaka 1959 hadi 1965 kisha akajiunga na Shule ya Sekondari Gamal Abdel Nassar mwaka 1966 hadi 1969, pia alisoma kidato cha tano na sita, katika Chuo cha Lumumba, Zanzibar kati ya mwaka 1970-1971.

Haji alisoma Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Elimu (BSC Education) kati ya mwaka 1972 hadi 1975. Baada ya kuhitimu aliajiriwa kama mwalimu wa Sekondari ya Beit Al Ras, wakati huo ikiitwa Gamal Abdil Nassir jina la Rais wa zamani wa Misri, baada ya mwaka mmoja alihamishiwa Sekondari ya Lumumba na kufundisha kidato cha tano na sita.

1978-1979, akasoma na kuhitimu stashahada ya juu ya elimu katika Chuo Kikuu cha Reading na aliporejea alihamishiwa Ofisi Kuu ya Wizara ya Elimu na kupewa wadhifa wa Ofisa Mipango ya Elimu.

Kabla ya kujiunga na Chama cha ACT-Wazalendo alikuwa mwanachama wa CUF. Akiwa CUF alishika nyadhifa mbalimbali kwa nyakati tofauti, ikiwamo Naibu Katibu Mkuu wa CUF Zanzibar na Mkurugenzi wa Uchumi na Fedha CUF Taifa mwaka 1999-2003.

Pia alikuwa Mkurugenzi wa Uchumi na Fedha CUF kati ya mwaka 1997-2010, Naibu Katibu Mkuu CUF Zanzibar kuanzia mwaka 1999 hadi 2010 na Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi Taifa CUF Taifa kati ya mwaka 1999-2014.

Mwaka 2015 Chama cha Wananchi CUF kilimteua mgombea nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika muungano wa UKAWA ambapo ilibidi ajiunge na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ili kukidhi matakwa ya kisheria ya kugombea nafasi hiyo ambapo mgombea wao wa urais wakati huo akiwa Edward Lowassa.

Wakati hayati Maalim Seif akitangaza kujiunga na Chama cha ACT-Wazalendo mwezi Machi 2019, alikuwa ni mmoja wa makada wa CUF waliohama na Maalim kujiunga na chama hicho huku akipewa nafasi ya kuwa Naibu Kiongozi wa chama na Maalim akipewa nafasi ya kuwa Mshauri Mkuu wa Chama.

# Viongozi CHADEMA watumbuliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kimevunja uongozi wake katika Wilaya ya Mbeya Mjini kutokana na wajumbe wake kufanya makosa mbalimbali ikiwamo kuvuruga mkutano wa kanda hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho Kanda ya Nyasa, Mwenyekiti wa Kanda hiyo, Mchungaji Peter Msigwa, alisema viongozi walioondolewa kwenye uongozi huo wapo 11 wakiongozwa na Mwenyekiti John Mwambigija.

Alisema viongozi hao waliongoza genge la wahuni kufanya fujo kwenye mkutano wa chama hicho kanda uliokuwa na lengo la kusuluhisha mgogoro uliokuwapo kati ya viongozi hao na wanachama.

Msigwa alisema wanachama wa CHADEMA Jimbo la Mbeya Mjini walikuwa wanawalalamikia viongozi hao kuwa wanawafukuza uwanachama bila kufuata utaratibu na waliwafukuza baadhi ya viongozi waliochaguliwa na wananchi.

Alisema baada ya taarifa za mgogoro huo kuufikia uongozi wa chama hicho kanda pamoja na maelekezo ya Taifa iliamuliwa Kamati Tendaji ya Kanda hiyo kwenda kusuluhisha na wakati mkutano wa usuluhishi unaendelea ndipo Mwambigija na wenzake walianzisha fujo.

Alisema kutokana na kufanya fujo hizo, kamati hiyo iliamua kuahirisha mkutano na ndipo vikafanyika vikao ambavyo viliamua wavuliwe uongozi na wabaki kuwa wanachama wa kawaida wakati taratibu zingine zikiendelea.

"Kwa mujibu wa taratibu za chama chetu maamuzi ya kinidhamu yanaanzia kwenye ngazi za chini na hawa walitakiwa washughulikiwe na ngazi ya mkoa, lakini tumechukua hatua hizi ngazi ya kanda kwa sababu walionyesha utovu wa nidhamu kwenye mkutano wa ngazi yetu," alisema Msigwa na kuongeza. "Mbali na kuwavua uongozi, tumewaandikia barua za kuwataka wajieleze ndani ya siku 14 kwanini wasifukuzwe uwanachama kutokana na vitendo vyao vya utovu wa nidhamu," alisema Msigwa.

Vilevile Msigwa alisema Kamati Tendaji ya Chama hicho Kanda ya Nyasa imeuelekeza uongozi wa chama hicho Mkoa wa Mbeya, kuunda kamati maalumu ndani ya siku tatu ambayo ndiyo itakuwa inaendesha shughuli za chama hicho katika wilaya hiyo.

Hata hivyo, alisema Kamati hiyo Tendaji ya Kanda iliuelekeza uongozi wa CHADEMA ngazi ya Mkoa wa Mbeya kuandaa uchaguzi wa kuziba nafasi za viongozi hao ndani ya siku 60 muda ambao alisema ni kwa mujibu wa katiba ya chama hicho.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwasote maarufu China wa China, alisema katika mkoa huo kuna majimbo saba, lakini lenye mgogoro ni la Mbeya Mjini pekee ambalo alisema limekuwa likiwaumiza vichwa.

Alisema wao wasingeweza kufanya maamuzi ya kinidhamu dhidi ya viongozi hao baada ya kufanya fujo hizo kwa sababu kikao hicho hakikuwa katika ngazi yao.

Alisema tukio walilolifanya viongozi hao liliwafedhehesha kutokana na kwamba wao ndio walikuwa wenyeji wa mkutano huo na kwamba walijiandaa toka mwanzo kwa kuhakikisha wanachama waliowafukuza hawaingii.

# Mchuano nafasi ya Naibu Spika bado kitendawili

**Na Salome Kitomari**

KINYANG'ANYIRO cha kumpata Spika wa Bunge kinatarajiwa kufika tamati kesho baada ya wabunge kupiga kura ya kumchagua kiongozi huyo kwa mujibu wa kanuni za Bunge za mwaka 2020.

Aidha, joto la uchaguzi huo lipo kwenye nafasi ya Naibu Spika, ambayo hadi sasa haijajulikana nani atashinda, baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumpitisha aliyekuwa Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, kugombea nafasi hiyo, iliyoachwa wazi na Job Ndugai aliyejiuzulu Januari 6, mwaka huu.

Nipashe ilimuuliza Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama hicho NEC (Itikadi na Uenezi), Shaka Hamdu Shaka, alipouliza kuhusu utaratibu wa kumpata Naibu Spika ndani ya chama hicho alisema: "Utaratibu haujatolewa."

Kwa mujibu wa kanuni za Bunge, spika anachaguliwa kwenye kikao cha kwanza baada ya kiti hicho kuwa wazi.

Kanuni hizo zinasema chama cha siasa kina haki ya kupendekeza jina la mbunge anayeweza kugombe anafasi hiyo, pia kinaweza kuchagua majina ya wagombea ambao si wabunge yatawasilishwa Tume ya Taifa Uchaguzi (NEC) siku tano kabla.

Aidha, kanuni hizo zinasema uchaguzi utasimamiwa na mwenyekiti ambaye atatoka miongoni mwa wabunge ambao wamekuwa mfululizo kwa muda mrefu na asiye mgombea wa nafasi hiyo baada ya kuombwa na Katibu wa Bunge kuongoza kikao hicho.

"Baada ya uchaguzi wa Spika kukamilika mwenyekiti atamuita Spika ajongee mbele ya Bunge ili aape viapo vitakavyowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni," anasema kanuni hizo.

Kwa Naibu Spika, utaratibu wa kumpata utafanyika mapema baada ya spika kupatikana na nafasi hiyo kuwa wazi na utaendeshwa kwa utaratibu ule ule wa kumchagua spika.

"Isipokuwa kwamba mbunge hawezi kushiriki uchaguzi wa naibu spika iwapo hajaapa kiapo cha uaminifu, aidha, mbunge yeyote atakayechaguliwa kabla ya kushika madaraka yake ataapishwa na spika mbele ya Bunge kiapo cha naibu spika," zinaeleza kanuni hizo.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# TANGAZO LA MNADA

Wananchi wote wanatangaziwa kwamba, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) watauza kwa njia ya Mnada wa Hadhara magari .

| TAREHE | KITUO | AINA YA VIFAA |
|---|---|---|
| 12/02/2022 | Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) – J.Nyerere Int'l Airport Term 1 Admin Block. | Toyota Landcruizer 5<br>Toyota Coaster 1<br>Toyo Tractor 1<br>Toyota Hiace 1 |

**MASHARTI YA MNADA:-**

1. Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa amana papohapo sichiniya asilimia ishirini natano (25%) yathamani ya Chombo/Kifaa alichonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14), kuanzia tarehe ya kifaa kunadiwa. Kushindwa kufanya hivyo kutamuondolea mnunuzi haki zote za ununuzi wa Chombo/kifaa kinachohusika na AMANA (Deposit) haitarudishwa;
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa sikusaba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;
4. Ruhusa ya kuangalia vyombo hivyo itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya Mnada;
5. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi.

**MKURUGENZI MKUU**
**KAMPUNI YA NDEGE TANZANIA (ATCL)**

## HABARI KITAIFA

# Wanasaikolojia wafunguka kasi mauaji

**Na Jenifer Gilla**

MFULULIZO wa matukio ya mauaji ya kutisha yanayoendelea na kuwaacha ndugu na jamaa wa waliouawa katika simanzi na sintofahamu, yamewaibua wanasaikolojia.

Baadhi ya matukio hayo ni la watu wa tano wa familia moja kuuawa, na watu wasiojulikana na kutelekezwa ndani ya nyumba hadi ilipotambulika na watu Januari 22, mwaka huu katika kijiji cha Zanka, Bahi, mkoani Dodoma.

Pia la kukatwa mapanga hadi kufa kwa mjamzito na watoto wake wawili huko Sumbawanga ambapo Jeshi la Polisi la mkoa huo linamshikilia Philipo Vicent (22) kwa tuhuma za mauaji hayo.

Kadhalika, Jeshi la Polisi mkoani Mara linawashikilia watu sita kwa tuhuma za mauaji ya bibi kizee, mkazi wa kijiji cha Rigicha, wilayani Serengeti, chanzo cha mauaji kikidaiwa kuwa imani za kishirikina.

Mfululizo wa matukio haya ulionyesha kumkera Rais Samia Suluhu Hassan, na kumtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, kuchukua hatua kukomesha vitendo hilo.

Pia aliwapa siku saba Polisi Mkoa wa Dodoma, Mkuu wa Mkoa huo pamoja na kamati ya ulinzi kuwakamata watu wote waliohusika na mauaji ya kikatili ya watu watano mkoani humo.

Nipashe iliwatafuta wanasaikolojia ambao walielezea chanzo cha matatizo hayo katika jamii katika mtizamo wa kisaikolojia.

Mwanasaikolojia ya Tiba kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Isac Lema, alisema kuwa kitendo cha mtu kujidhuru au kumdhuru mwezie si cha kawaida, kinatokana na msukumo ulioko ndani yake, ambao huchochewa na mabadiliko ya tabia.

Alisema hali ya mabadiliko ya tabia hutokana na mambo mbalimbali kama vile kuhamaki (kutenda jambo pasipo kufikiria), migogoro aidha ya muda mrefu au mfupi ambayo hupelekea mtu kupata kiwango kikubwa cha msongo wa mawazo.

"Migogoro husababisha vibebeo vikubwa viwili vya msongo wa mawazo ambavyo visasi, chuki za muda mrefu. Sasa chuki na visasi vikizidi kupiliza ndivyo humsababisha mtu kufanya vitendo visivyotarajiwa, na hii hutokana na mtu kushindwa kuhimili hali ya msongo wa mawazo aliyonayo," alisema.

Kupunguza vitendo vya mauaji kuendelea kutokea msaikolojia huyo anashauri jamii ihamasishwe kuchunguza afya ya akili mara kwa mara kwa sababu husababishwa na matukio yanayoendelea katika jamii.

"Kuchunguza afya ya akili si tu kuangalia kama una ugonjwa wa akili bali ni kuangalia tabia zetu na vitu vinavyopelekea mabadiliko ya tabia zetu mfano matumizi ya vilevi kupita kiasi kama pombe, bangi kwa sababu vitu hivi vinapelekea kuwapo kwa matukio ya jinai, "alifafanua.

Alishauri pia kutatua migogoro ya kijamii kwa wakati, kwa sababu ikiachwa kwa muda mrefu ndio hutengeneza chuki na visasi na hasira ambavyo navyo vikikomaa ndio hupelekea mtu kufanya vitendo vya kikatili.

Alisema kuwa katika hali kama hii afya ya akili ndio inahusika lakini sio ugonjwa wa akili, na wengi waliofanya vitendo kama hivi wakipelekwa kupimwa hawakutwi na viashiria vya ugonjwa wa akili.

Naye Msaikolojia Tiba, George Chacha alisema kuwa kuna uwezekano mkubwa kuwa matukio haya yalikuwapo tangu zamani isipokuwa sasa kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na elimu waliokuwa nayo watu yamekuwa yakiripotiwa na taarifa kuenea kwa watu wengi ndani ya muda mfupi.

"Hata ukisoma ripoti kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) na ile ya Hospitali Kuu ya Magonjwa ya Afya nchini MIREMBE, zinaonyesha kuwa Tanzania ina watu takribani milioni saba wanaougua afya ya akili, hii inaonyesha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kufanyika vitendo ambavyo haviendani na haki za binadamu ikiwamo mauaji," anaelezea George.

Aliesema pia malezi yanaweza kuchangia kuwapo kwa matukio haya katika jamii, mzazi anapaswa kukemea tabia au mienendo mibaya ya mtoto tangu akiwa mdogo, kwa sababu akikuwa na tabia hizo nazo zinakuwa na kufikia hatua ya kufanya vitendo viovu ikiwamo mauaji.

"Mfano kunakesi zinazohitaji subira, kama zile zinazohusisha mgawanyo wa mali, watoto ambao hawajakuzwa katika misingi mizuri ndio wanakuwa wakwanza kukwazika kwa kukosa uvumilivu kwa tamaa za mali hali inayopelekea kufanya vitendo hivi,"anasema.

Alirejelea tafiti zilizofanyika hivi karibuni zinazoonyesha kuwa hali ya utu wa kumjali mtu mwingine kwa sasa zimepungua kwa asilimia 40 ukilinganisha na miaka ya1980.

DK. Saldeen Kimangale, Mwanasaikolojia tiba kutoka Hospitali ya Somedics Polyclinic Health Centre ya jijini Dar es Salaam, alisema kuna haja ya kufanyika tafiti ili kufahamu kwa nini matendo haya yameshamiri kwa sasa katika jamii.

"Zipo theory (dhana) mbalimbali zinazoonyesha kwanini mtu anafikia hatua ya kufanya mauaji kwa mfano , mama kumuua mtoto wake kisha na yeye kujiua, kila theory ikitoa sababu zake kama vile umri, jinsia, afya ya akili kwa hivyo ni muhimu kufanya utafiti ili kufahamu ni kitu gani kinapelekea matendo haya ya kikatili kushamiri kwa sasa.

Sisi kama wataalamu wa magonjwa ya akili matukio ya namna hii tunayaweka kama sehemu ya afya ya akili kwa sababu si kila mtu anaweza kufikia hatua ya kutoa uhai wa mwenzie kwa sababu yoyote ile, kunakuwa na msukumo ndani yake ambao unapelekea kufanya kitu hicho ," anasema Dk. Saldeen.

Aliutaja utoaji taarifa wa matukio haya kiholela unaweza kuchagiza mtu mwingine kufanya tukio akidhani kuwa ndivyo uhalisia. Ili kutamka kwamba huu ni ugonjwa wa akili au ni mgonjwa wa akili lazima ithibitishwe na daktari bigwa wa afya na magonjwa ya akili.

Anasema pia kuna baadhi ya magonjwa kama kama vile 'depression' sonona huchangia watu kujitoa uhai wao au kutoa uhai wa mwenzie.Pia suala la kutoa taarifa za mauaji ya watu kiholela mbele ya watoto wadogo, huwajengea watoto wao ujasiri kuwa ni jambo la kawaida nao wanakuja kuendeleza tabia hizo wakija kuwa wakubwa.

"Unakuta mtu anafurahia mbele ya watoto wadogo kitendo cha mwizi au kibaka kupigwa hadi kutolewa uhai na wananchi, taarifa kama hizi zinajengeka katika akili ya mtoto na zinakuja kuwa tabia pindi anapokuwa mtu mzima, ni kama vile mtoto akiwa anashuhudia mama yake anapigwa na baba yake kila mara, naye akiwa mkubwa anakuwa anampiga mke wake," anafafanua.

Kuzuia haya yasitokee Dk. Saldeen ameshauri serikali itoe kipaumbele katika uwekezaji katika afya na magonjwa ya akili ikiwamo elimu ya afya na magonjwa ya akili iwepo kwenye mitaala ya shule za msingi na sekondari na pia itolewe kwenye kliniki ya mama na mtoto hasa kujua vihatarishi na viashiria ukatili.

Ameshauri pia mamlaka na vitengo vya serikali kama public health, social workers, community health worker, wataalamu wa afya na magonjwa ya akili, Jeshi la Polisi, wadau wa haki za binadamu wawe na forum ya kujadili kadhia hii na kuweka mikakati na miongozo ya kuzuia ukatili huu.

# Mwanafunzi anusurika ndoa kwa mahari ya ng'ombe 14

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MWANAFUNZI aliyefaulu kuingia kidato cha kwanza mwenye umri wa miaka 15 (jina linahifadhiwa) wilayani hapo, amesimulia alivyonusurika kuozeshwa ndoa ya utotoni na baba yake mzazi kwa mahari ya ng'ombe 14.

Akisimulia mkasa wa tukio hilo, mwanafunzi huyo aliiambia Nipashe kuwa baba yake anaishi mkoani Tabora na mwanamke mwingine baada ya kuwatelekeza.

Alisema huwa anarudi nyumbani kwa ajili ya kuwaozesha binti zake na kuondoka na mifugo na ameshafanya hivyo kwa dada zake wawili kwa mtindo huo na sasa wanaishi kwa mateso.

Mwanafunzi huyo alisema baba yake alifika nyumbani na kumwambia hakuna kwenda shule kwa kuwa anataka kumuozesha na ameshatolewa mahari ya ng'ombe 14, ndipo alipoamua kuazima baiskeli kwa jirani na kukimbia hadi kwa mtendaji wa kata umbali wa zaidi ya kilomita 10 kutoa taarifa.

"Mimi sitaki kuolewa, sababu nimeshuhudia dada zangu wawili ambao baba aliwaozesha na kuwakatisha masomo, wanaishi maisha magumu sana, nataka nisome ili nitimize ndoto zangu za kuwa mwalimu nisaidie wadogo zangu," alisema.

Mama mzazi wa mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa) alikiri mume wake kuitelekeza familia yake na kurudi nyumbani kuozesha watoto na kuondoka na mali yote.

Mama huyo aliiomba serikali imsaidie mwanawe asome ili aje amsaidie baadaye kuwa wanaishi maisha magumu.

Alisema kwa sasa mtoto wake huyo, amempeleka katika Shirika la Agape mjini Shinyanga, ambalo lina nyumba salama ya watoto wenye madhira ya ndoa za utotoni, kwa ajili ya usalama wake kwa hofu baba yake anaweza kumfuata usiku na kuondoka naye kwa nguvu.

Mtendaji wa Kata ya Pandagichiza, Deogratius Mashamba, alisema baada ya mwanafunzi huyo kufika kwenye ofisi hiyo, aliwasiliana na Dawati Jinsia la Polisi ili wakamkamate baba huyo, lakini alitoroka usiku wa manane kusikojulikana na wanaendelea kumtafuta kwa kushirikiana na polisi.


**KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI**

BAHARI BEACH HOTEL LTD inatangaza kupotea kwa kadi za magari zenye namba za usajili T 962 BUL, T 684 BSC, T 655 BSC, T 680 BSC, T 487 AJP, T 532 BSH, T 428 AVE na T 700 ASZ. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi: KW/RB/325/2022.

**TANGAZO LA KUUZA CALENDAR**

Tunaunza calendar mashine moja Simtank 4 zenye ujazo wa lita 15,000 kwa moja Na desalination plant

*Kwa mawasiliano zaidi piga +255 784 282 995*

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**DIANA CHRIZOSTOM RUTTA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 764 ASA – SUZUKI ESCUDO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/40228/2022.**


*Magistrates Court( Approved Forms For the Primary Court)*

**GN. NO 943(Contd.)**
**FOMU MIRATH-2**
**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANI**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Lembeni –Wilaya ya Mwembe**
**Kituo cha Lembeni Mkoa wa Kilimanjaro**
**Usimamizi wa mirathi Na, 01/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**Marehemu Veronica Kighenda Mdee wa Kilomeni**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUWA MSMAMIZI YALIYOYOLETWA**
**NA GRACE VENANCE MDEE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 mwezi 01 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
*Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 14 mwezi 01mwaka 2022**

.............................
**HAKIMU**

# Pyxus Agriculture Tanzania Limited: The factory behind sunflower farmers successes

IT is undeniable fact that when it comes to production of edible oil, sunflower growers have a significant role to play, in terms of providing the much needed raw material.

For the past three consecutive years Tanzania has been haplessly grappling with the acute shortage of edible oil, among others, due to poor production and productivity in the production of sunflowers.

In Tanzania, sunflowers contributes to at least 68.9 percent of all edible oil produced, whereby the remaining 30.1 percent are coming from other crops, including palm oil.

Established and registered on 30 November 2018, the Pyxus Agriculture Tanzania Limited is specifically focused to support the sunflower farmers from across the country by providing them with a viable market for their produce.

The main objective is also to allow the growers to expand and further diversify and increase their livelihood.

" As part of diversification strategy, the company has from December 2018 contracted, and will continue to enter into patriotic contracts with commercial and smallholder farmers within the country to grow sunflower seeds that will be processed at our newly acquired and upgraded Edible Oil mill and refinery in Dodoma region," expressed the Company's Managing Director, Mr. Malcolm McGrath.

He informed that during the crop year 2020, the reputable company sealed contracts with at least 4,800 sunflower growers in Tanzania, added: "This has played a key role in helping to promote employment in the community by engaging into the farming activities,"

He detailed that, in a robust project to assist the farmers, Pyxus Agriculture Tanzania Limited separates the growers into three categories.

" The first category involves the smallholder farmers (AMCOS and registered groups) owning 1.5 to 5 hectares of land, whereby the second category attracts the farmers with from 5 to 80 hectares," he expressed.

Moreover, he said the third group is of the commercial growers who possesses over 80 hectares.

" The contracted farmers are based in Dodoma, Manyara, Iringa, Kiteto, Morogoro, Tanga, Tanga, Magu, Kilimanjaro and Singida regions," he informed, adding that most of the commercial farmers were from Katesh, Simanjiro as well as Babati.

Giving more details, Mr. McGrath said the company has a strong and well-planned agronomy support structure, logistics' infrastructure and support system in place within Tanzania that are used to ensure and improve farmer's performance and their incomes.

Following a set- strong support system on the extension services that the company rolled- out to it's growers, and linkage so far created, he said most farmers have been attracted and keen to work with Pyxus Agriculture Tanzania Limited.

" The company continually trains it's contracted farmers on how best to increase productivity and yields, the development which enable them to fetch more profit," he observed.

He disclosed some of the key agro-practices that the farmers are being imparted with as professional application of fertilizer, planting spacing as well as use of improved and hybrid seed varieties.

" We're seriously supporting and encouraging indigenous farmers to embark on large plantation of sunflower seeds in order to curtail a sharp shortage as statistics depicts that the country imports between 50 to 60 percent edible oil due to shortage," the director added.
He assured that the esteemed company will continue to encourage and lead the growers to adopt good agronomic practices, including fertilization and use of mechanical farming implements in order to boost farmers productivity and yields.

However, despite putting helpful system of getting enough raw materials for the factory, he expressed grave concern over failure by the farmers to provide needed tonnage of sunflower grain seed.

" The factory's annual demand for sunflower grain seed stands at 20,000 metric tons (MT) but the contracted farmers have yet to cater as per the demand as we're experiencing a shortage of 50 percent," he unveiled.

To mitigate the challenge, he said the company has decided to buy crude oil from smallholder processors and refine it to standard edible oil.

Apart from that, he expressed concern at the tendency by some contracted farmers to market their produce out of the contract.

" It's very challenging as some farmers are failing to adhere to the selling and buying contract by selling their produce to third parties even though there's a contract agreeing to sell to Pyxus Agriculture Tanzania,"



Pyxus Agriculture Tanzania Limited Managing Director, Mr Malcolm McGrath displays the edible oil brand 'Golden Harvest' which is produced by the company.

To that end, he said the company was seeking support from the parent ministry in order overcome these challenges.

Mr McGrath spoke over other challenge, saying imported oil is permitted to land in Tanzania at a very low price, observed: "This brings difficulties to local producers who work directly with growers and provide services to them,"

Unreliable supply of safe water was a challenges he also said frustrated the company in running it's production activities smoothly.

The company is a producer of the high quality and favorable edible oil, dubbed 'Golden Harvest (pure sunflower oil).
" Our brand is equal to imported ones and we have so far fetched good markets in Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza and Dodoma," he informed.

He said plans are afoot for the company to extent it's market foothold to neighboring countries of Uganda, Kenya, Rwanda and DRC Congo, to mention but a few.

Dwelling over the company's future plans, he said the modern plant plans to expand its production scope from the currently 20,000MT to at least 40,000MT in a period of five years to come.

" Our current annual seed processing capacity is at 20,000 MT which produces approximately 6,000MT (6.6 million liters) of refined fortified sunflower oil," he stated.

Contrary to many other like- minded factory, he said the company was using high oil refining process which includes deodorization, neutralization, fortification and winterization (20MT/24 hours).

On his side, the company's smallholder farmers manager, Mr. Edwin Shio, said the farmers have been introduced to best sunflower varieties, which involves mixture of improved and Open Pollinated Varieties (OPV).

He named the seeds as Hysun 33, Aguara 4 and 6, SuperSun 66, Ancilla, Michele and Improved Records.

" The objective is to ensure the farmers are getting good yields, but also produce grain seeds with high oil content," he said.

And he observed, most of the planting seed sold and supplied to farmers in Tanzania is imported and sold at high prices which most growers cannot afford.

With good relationship with different financial institutions, he said Pyxus Agriculture Tanzania Limited will continue link it's contracted farmers to secure lucrative financial agricultural support.

" For instance, CRDB Plc, the Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) and NMB have shown interest and readiness to support the farmers at diverse tunes," he unveiled.

With the best agronomic practices, he said the farmers were expected to yield up to 1,500MT per hectare.

On the same vein, he said the company in partnership with other agro-stakeholders was implementing a special project to assist the farmers in Kongwa, Mpwapwa and Kiteto to produce sunflower organically.

" We're implementing the project with an eye to start producing edible oil from the organically produced sunflower grain seeds, but the products will specifically be for exportation," he informed.

Pyxus Agriculture Tanzania Limited employs over 390 staffs on both, permanent and seasonal basis through it various sunflower operation around the county.

According to the Tanzania Investment Centre (TIC) oil demand for consumption in Tanzania is 600,000MT per annum.

The country produces only 180,000MT of edible oil forcing it to import 420,000MT and it is forecasted that demand would increase to 700,000MT by 2030.

Locally produced sunflower oil can only cover the gap of importation through improved yields, modern infrastructure and if all challenges will be resolved.

We need to have a perfect market to cater the consumers where all standards are common and effectively enforced, this will enable local market to have highest of qualities that are locally manufactured. Consumers should determine what to buy based on quality and value addition.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TPLB ongezeni makali zaidi kwa waamuzi hawa Ligi Kuu

**MCHAKAMCHAKA** wa Ligi Kuu Tanzania Bara mzunguko wa 14 utanza wiki hii baada ya mwishoni mwa wiki kupisha mechi za hatua ya 32 ya michuano ya Kombe la FA, ambayo bingwa huiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Mzunguko wa 14, utaanza wakati Yanga ikiendelea kutesa kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 10 zaidi ya Mabingwa Watetezi, Simba wenye alama 25 katika nafasi ya pili ya ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.

Hata hivyo, ligi hiyo ambayo msimu huu imekuwa ngumu zaidi tofauti na misimu mingi iliyopita, inaendelea huku kilio kikubwa kikielekezwa kwa waamuzi kushindwa kutafsiri vema sheria za mpira wa miguu kwa kutokujua, mapenzi binafsi kwa baadhi ya klabu au pengine kwa kurubuniwa ama vinginevyo.

Hata hivyo, wiki iliyopita Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) katika kikao chake cha Januari 27, mwaka huu kilipitia mwenendo na matukio mbalimbali na kufanya maamuzi kadhaa ambayo pia yaliwakumba baadhi ya waamuzi.

Waliokumbwa na maamuzi hayo ya Kamati ya TPLB, ni Mwamuzi wa Kati, Hance Mabena kutoka Tanga, ambaye ameondolewa kwenye ratiba ya waamuzi kwa mizunguko mitatu kwa kosa la kushindwa kutafsiri vema sheria za mpira wa miguu kwenye tukio la mchezaji wa Yanga, Djuma Shabani kuchezewa rafu kabla ya kulipiza kwa kumpiga kiwiko, mchezaji wa Polisi Tanzania, Yahaya Mbegu. Katika mchezo huo wa Ligi Kuu raundi ya 13 uliopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, pia Mwamuzi Msaidizi namba moja, Pascal Joseph kutoka Shinyanga na mwamuzi wa akiba, Jackson Samweli wa Arusha, wameondolewa kwenye ratiba ya waamuzi kwa mizunguko mitano kwa kosa la kushindwa kumsaidia mwamuzi wa kati, Mabena katika kutafsiri vema sheria za mpira wa miguu kwenye tukio hilo la Djuma.

Kwa ujumla tunaipongeza TPLB kwa kuchukua hatua hizo ambazo tunaamini itakuwa fundisho kwa waamuzi wengine ambao wanafinyanga sheria za soka na kuziacha timu zingine zikilia kwa kupoteza pointi visivyo halali.

Hata hivyo, tunaitaka TPLB iendeleze wimbi hili kwa kutosita kuchukua adhabu kali zaidi, kwani kwa tukio kama alilolifanya Djuma hadi yeye mwenyewe akajutia pamoja na klabu yake, kabla hata ya adhabu hizo ambapo naye amefungiwa mechi tatu na faini ya shilingi milioni moja, ni dhahiri waamuzi wetu wanapaswa kuchukuliwa hatua kali zaidi kwani kwa kufumbia macho matukio kama haya, ipo siku tutashuhudia madhara makubwa zaidi kwa afya za wachezaji ama hata kupoteza maisha uwanjani.

Nipashe hatutaki kuona madhara makubwa zaidi yakitokea, hivyo njia pekee ya kudhibiti matukio kama hayo ni umakini zaidi kwa waamuzi huku wakichezesha kwa haki, lakini TPLB kutosita kuchukua hatua kali kwa wote wanaofinyanga kanuni/sheria za soka. Tunaamini TPLB ikiongeza umakini na kutosita kuchukua hatua kali kwa waamuzi wanaovurunda ligi yetu itakuwa bora zaidi na ushindani utaongezeka huku akipatikana bingwa aliyestahili atakayeweza kwenda kutoa ushindani wa kweli kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.


Aidha, hatuna budi kuwasihi waamuzi kuongeza umakini na kutosita kutoa kadi nyekundu hata tatu ama zaidi pale inapolazimika kufanya hivyo kutokana na makosa ya wachezaji uwanjani.

Tunatambua mara nyingi wamekuwa wakilazimika kuongozwa na busara zaidi ama mapenzi yao au vinginevyo badala ya kufuata sheria/kanuni zinazoongoza mpira wa miguu duniani, hivyo kusababisha rafu nyingi zinazoweza kuhatarisha afya za wachezaji, katika hilo tunataka haki itendeke si kutenda tu bali pia ionekane ikitendeka kweli.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi Bongo jifunzeni kwa Komba

Na Adam Fungamwango

**KUMWONEA** mtu wivu si lazima umfanyie kitu kibaya, la hasha, ila unaweza kuongeza bidii na kufanya kama anavyofanya yeye au zaidi ili mradi uwe kama yeye kujifunza na kufanikiwa kupitia kwake.

Ndiyo, nasema hivyo kwa sababu kuna watu wengine wao wakimwonea mtu wivu, basi kinachofuata ni fitina na mambo mengine yanayofanana na hayo ili kumkwamisha ama kumshusha.

Kwa sasa kwenye soka la Tanzania si siri kwamba upande wa waamuzi unabebwa zaidi na mwamuzi wa kimataifa, Frank Komba.

Hatuwezi kuendelea na kuandika chochote, bila kwanza kumpa pongezi zake, kwani mpaka sasa yupo nchini Cameroon akiwa mmoja wa waamuzi kwenye michuano hiyo.

Ndiye mwamuzi pekee kutoka Tanzania amekuwa akiiwakilisha vema, kwani tangu achaguliwe, hatujasikia chochote kibaya, au malalamiko kuwa amechezesha vibaya.

Wakati yupo nchini Cameroon akiwa mmoja wa waamuzi wa fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), kwa mara nyingine tena Shirikisho la Soka Afrika (CAF), limemteua mwamuzi huyo bora kabisa kwa sasa nchini, Komba, kuwa miongoni mwa waamuzi watakaochezesha mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi kati ya Raja Casablanca ya Morocco na Amazulu ya Afrika Kusini, utakaochezwa kwenye Uwanja wa Mohamed wa Tano unaotarajia kupigwa Februari 12, mwaka huu.

Kwa muda mrefu wadau wa soka wamekuwa wakilalamika ni kwa nini wachezaji wengi wa Kitanzania hawaendi kucheza soka la kulipwa nje ya nchi na badala yake mpaka leo bado watu wanaimba wimbo wa Mbwana Samatta na Simon Msuva, huku baadhi yao wakienda lakini baada ya muda mfupi wanarejea hapa hapa.

Mjadala huu nao uligeuka baada ya wengine kudai hata waamuzi wa Tanzania wamekuwa hawateuliwi kuchezesha michuano mbalimbali ya kimataifa tofauti na zamani ambapo wengi kama kina Hafidh Ally, Dastan Daffa, Manyoto Ndimbo, Leslie Liunda, Ally Juma David, Omary Abdulkadir, Gratian Matovu na wengineo ambao waliipeperusha vema bendera ya Tanzania nje ya nchi kwa kuchezesha michuano mbalimbali ya kimataifa ndani na nje ya nchi.

Tanzania iliheshimika kwa kuwa na waamuzi wengi bora kabisa kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati, lakini kwa sasa mambo yamebadilika. Baadhi ya waamuzi wa Tanzania wamekuwa wakichezesha soka kwa namna ambayo unashindwa kuelewa.

Kosa la wazi ambalo wala halihitaji mjadala, na wala hata asiyejua vizuri mambo ya soka na sheria zake, anaweza kutoa uamuzi kama ni penalti, kadi nyekundu au adhabu, wakati haistahili pale inapostahili hatekelezi hilo. Tena inawezekana akawa yupo karibu zaidi na tukio kuliko mtu yeyote, lakini akajibaraguza kama hajaona.

Inashangaza kuona waamuzi wengi sasa wanakubali kutawaliwa uwanjani na wachezaji, badala ya wao kuutawala mchezo. Mwamuzi anaweza kusukumwa mpaka anataka kuanguka na wachezaji, lakini huwezi kumuona anachukua hatua na hasa kama wanaofanya hivyo ni wachezaji wa timu kubwa zenye mashabiki wengi.

Huwezi kuwa mwamuzi bora kama huwezi kuitawala mechi na wachezaji wote kama wanavyofanya wenzetu na badala yake kuwaacha wachezaji wakutawale na kujifanyia chochote wanachotaka uwanjani.

Kwa bahati mbaya sana kwa sasa Ligi Kuu ya Tanzania inaonyeshwa mubashara, hivyo sidhani kama wakubwa wa waamuzi Afrika wanaweza kuwachagua waamuzi dhaifu wa Tanzania ambao wanachezesha kwa woga na kwa hisia, badala ya sheria za soka zinavyotaka.

Nadhani sasa inabidi waamuzi wa Tanzania waanze kubadilika ili kuwe na kina Komba wengi huko kimataifa. Inawezekana rushwa, mapenzi ya timu, woga wa mashabiki, woga wa kukosolewa kwenye mitandao ya kijamii na wachambuzi, ndivyo vinavyowafanya waamuzi kutofanya vema, lakini unapotaka kuwa bora huna sababu ya kuogopa kelele za wasiojua sheria/ kanuni za mchezo husika.

Cha kufanya wao wachezeshe kwa kufuata sheria tu wasiogope chochote. Hata Komba mwenyewe wachambuzi walimsema sana kwenye mechi moja ya msimu uliopita ya Simba na Yanga, alipotoka pembeni kwenye mstari na kuingia ndani ya uwanja, kukimbia sambamba na mchezaji wa Simba aliyekuwa anakwenda kushambulia. Wakati wachambuzi na mashabiki wanamshambulia kwa maneno ya kejeli, kumbe wakaja kuambiwa kuwa ni kanuni mpya ya soka iliyotoka hivi karibuni, kila mtu akakaa kimya. Hongera Komba, waamuzi Tanzania waige mfano wako.

## TANGAZO

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31-12-2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 31/12/2021 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 30/09/2021 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 841 | 887 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 86 | 66 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 3,651 | 2,910 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 15,051 | 14,296 |
| 12 | Mali nyingine | 4,229 | 4,272 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 569 | 554 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **24,426** | **22,985** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 15,265 | 14,745 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 1,142 | 337 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 409 | 490 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 485 | 544 |
| 28 | Madeni | 2,586 | 2,586 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **19,891** | **18,705** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **4,535** | **4,280** |
| | | - | - |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | 8,789 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | - | - |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (5,280) | (5,278) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 933 | 668 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | 93 | 101 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | | |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **4,535** | **4,280** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,562 | 1,959 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,051 | 1,051 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 18.57% | 18.62% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 9.70% | 13.70% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 91.72% | 94.76% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 61.62% | 62.19% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 82.06% | 87.79% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 8.78% | 2.77% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 6.27% | 2.37% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-12-2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 31/12/2021 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31/12/2020 | Limbikizo lamwaka sasa 31/12/2021 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 31/12/2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 914 | 964 | 3,871 | 3,836 |
| 2 | Gharama za Riba | (113) | (278) | (656) | (959) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | **801** | **686** | 3,215 | 2,877 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (139) | (119) | (374) | (188) |
| | | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | 221 | 227 | 831 | 779 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | **197** | **177** | 748 | 779 |
| | 6.3 Gawio | | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 24 | 49 | 12 | - |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | **(618)** | **(554)** | **(2,739)** | (2,652) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (317) | (269) | (1,344) | (1,366) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (45) | (41) | (213) | (132) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (256) | (244) | (1,182) | (1,154) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **265** | 240 | 933 | 816 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (30) | (48) | (90) | 100 |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **235** | 192 | 843 | 716 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **235** | **192** | **843** | **716** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 54 | 59 | 60 | 59 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 7 | 6 | 26 | 22 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 1.12% | 1.03% | 3.93% | 4.09% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 6.01% | 4.54% | 21.16% | 60.55% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 54.50% | 56.47% | 58.25% | 61.54% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 4.24% | 3.98% | 17.01% | 20.52% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho
kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31-12-21

(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,887** | **(5,280)** | **87** | **3,694** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 933 | - | **933** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | (91) | - | - | **(91)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,796** | **(4,347)** | **87** | **4,536** |
| | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 2,763 | (4,116) | 24 | **(1,329)** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 716 | - | **716** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | 6,124 | - | - | **6,124** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | **-** |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | (1,817) | - | **(1,817)** |
| Mengineyo | - | (63) | 63 | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,887** | **(5,280)** | **87** | **3,694** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-12-2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 31/12/2021 | Robo ya Mwaka iliyopita 30/09/2021 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31/12/2021 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31/12/2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 265 | 304 | 933 | 817 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | Hasara Katika Mali | 183 | 156 | 573 | 414 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (755) | 1,168 | (1,090) | (984) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,325 | 491 | 1,212 | 608 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (109) | 88 | (320) | 437 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 55 | (547) | (632) | (989) |
| | Kodi Iliyolipwa | (30) | (30) | (90) | (38) |
| | Mengineyo (Bainisha) | (158) | (56) | (348) | (448) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **775** | **1,573** | **238** | **(183)** |
| | | | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | | | | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (52) | (31) | (83) | (92) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(52)** | **(31)** | **(83)** | **(92)** |
| | | | | | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | (100) | (200) | (200) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | 5,000 |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | (2,077) |
| | Mengineyo (bainisha) | (10) | (83) | (91) | |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **(10)** | **(183)** | **(291)** | **2,723** |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 713 | 1,359 | (136) | 2,448 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 3,864 | 2,506 | 4,714 | 2,266 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **4,577** | **3,864** | **4,577** | **4,714** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Philip Raymond<br>Meneja Mkuu | (Imesainiwa) | **25/Jan/2022** |
| Kelvin Mushi<br>Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | (Imesainiwa) | **25/Jan/2022** |
| Saleh S. Abdallah<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | (Imesainiwa) | **25/Jan/2022** |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| Jina | | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Prof. Dominicus Kasilo<br>Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | (Imesainiwa) | **25/Jan/2022** |
| 2. Kitova Mungai<br>Mkurugenzi | (Imesainiwa) | **25/Jan/2022** |

### DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2015

### MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 1,800 |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account (GS09)** | |
| Account opening minimum amount | Free |
| Minimum operating balance | Free |
| Minimum Interest Bearing balance | N/A |
| Cash Withdrawal Fee | Refer cash withdrawal fee below |
| Credit Interest Rate | N/A |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 1,800 |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 10,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 1,800 |
| Interest Rate | |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |
| Prematurity withdrawals | 10,000 |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | Rate |
|---|---|
| 3 months | 4% |
| 6 months | 5% |
| 12months | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs**10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

**GENERAL CHARGES AND FEES**

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 1,500 |
| Cash withdrawal- from Tzs 5,000,000 and above) | 0.08%, Max Tzs 150,000 |
| Account closure | 10,000 |
| Dormant account reactivation | 5,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,500 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Bank Statement Fee /page | 1,200 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balance Inquiry | 200 |
| Money Transfer | 15,000 |
| ATM card Cost | 15,000 |
| Searching Fee | 10,000 |
| Coins deposit fee | 10% |
| ATM card replacement | 10,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,300 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,300 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alart | 500 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |
| ATM Balance Inquiry | 200 |

**LOAN CHARGES AND COMMISION**

| S/NO | CHARGIES |
|---|---|
| 1. | -Loan processing fee 2%<br>-Loan application fee 20,000/= |

TANGAZO

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.12.2021

### Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 31-Dec-21 | Robo Mwaka ya 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,150 | 6,571 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 15,835 | 24,017 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 28,691 | 19,182 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,967 | 17,159 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 31,099 | 31,026 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 71,174 | 66,148 |
| 12 | Mali Nyingine | 22,415 | 10,984 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,937 | 2,045 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **180,270** | **177,133** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 25,459 | 9,302 |
| 18 | Amana za Wateja | 113,060 | 119,254 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 9,339 | 12,802 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 32 | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,542 | 1,968 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,272 | 1,175 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,710 | 4,978 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **155,414** | **149,479** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **24,856** | **27,655** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (37,053) | (37,053) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,385 | 4,184 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **24,856** | **27,655** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 945,310 | 1,002,626 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,228 | 4,149 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 168 | 354 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 14% | 16% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.88% | 6.24% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 59% | 50% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 39% | 37% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 73% | 66% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -7% | 41% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2% | 0% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Dec-21 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,859 | 3,144 | 11,916 | 13,516 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,025) | (1,223) | (4,053) | (4,259) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,834** | **1,922** | **7,863** | **9,256** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | (165) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **119** | **2,510** | **9,361** | **9,075** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 364 | 413 | 1,346 | 1,428 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | (254) | 2,074 | 7,893 | 7,604 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 9 | 24 | 123 | 43 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(4,786)** | **(3,765)** | **(15,698)** | **(14,630)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,866) | (1,744) | (6,841) | (6,573) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (413) | (270) | (1,400) | (1,155) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (2,507) | (1,751) | (7,457) | (6,902) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(2,832)** | **667** | **1,526** | **3,537** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 34 | (120) | (141) | (92) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(2,799)** | **548** | **1,385** | **3,445** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(2,799)** | **548** | **1,385** | **3,445** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 128 | 124 | 128 | 114 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (445) | 87 | 220 | 548 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 7 | 7 | 7 | 5 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.57% | 0.31% | 0.78% | 1.78% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -10.66% | 1.98% | 5.28% | 16.26% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 160.67% | 66.58% | 73.78% | 64.76% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.48% | 1.65% | 6.36% | 2.01% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 31-Esfand-21 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Azar-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-20 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **(2,799)** | **548** | **1,385** | **3,445** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 639 | 456 | 639 | 1,783 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 5,027 | 5,298 | 15,229 | (13,941) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | (2) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 6,501 | (238) | 9,275 | (5,999) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 9,509 | 8,887 | 4,684 | 63,637 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,268) | 167 | 2,890 | (2,788) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 11,430 | (713) | 17,244 | 8,000 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | (61) |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **29,040** | **14,405** | **51,347** | **54,074** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | 295 | (372) | 4,875 | (225) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **295** | **(372)** | **4,875** | **(225)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 29,916 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **-** | **-** | **-** | **29,916** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **29,334** | **14,033** | **56,222** | **83,765** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 118,247 | 104,214 | 104,214 | 12,009 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **147,582** | **118,247** | **160,436** | **95,774** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,053) | - | - | - | 23,471 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,385 | - | - | - | 1,385 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(35,668)** | **-** | **-** | **-** | **24,856** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka uliopita 2020** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (40,498) | - | - | - | 20,026 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 3,445 | - | - | - | 3,445 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(37,053)** | **-** | **-** | **-** | **23,471** |

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| 1 | Gbenga Makinde<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | ***Imesainiwa*** | *31st January 2022* |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | ***Imesainiwa*** | *31st January 2022* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | ***Imesainiwa*** | *31st January 2022* |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | *31st January 2022* |
| 2 | Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | *31st January 2022* |

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa , USA and Europe .

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

## HABARI KITAIFA

# Maofisa ugani wakumbushwa majukumu

**Na Felix Andrew,** RUANGWA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, amesisitiza ushirikiano wa wadau katika kuendeleza kilimo, ambayo ni sekta mama ya uchumi wa Tanzania. Alisema hayo wilayani Ruangwa mkoani Lindi, alipokuwa akifunga awamu ya kwanza ya mafunzo rejea maalum kwa maofisa ugani yaliyotekelezwa katika mikoa 18 ya Tanzania Bara.

Mafunzo hayo yanayolenga kuongeza tija katika kutoa huduma za kilimo bora kwa wakulima ni juhudi za pamoja za wizara na taasisi ya uboreshaji mifumo ya masoko kwenye sekta za kilimo ya AMDT.

Mavunde alisema serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imejizatiti kuboresha uwezeshaji na utoaji wa huduma muhimu kwa wakulima, hususan wadogo, ili kuongeza uzalishaji na uongezaji thamani kwa mazao ya kilimo nchini.

Kilimo ni sekta mama kwa uchumi wa Tanzania kwa sasa ndio nguzo ya ajira, lishe, usalama wa chakula na inatuletea fedha nyingi sana za kigeni. Lakini kwa tulipofikia, tunatakiwa kuendesha kilimo cha kisasa na chenye tija ya hali ya juu sana ili kuwa na ushindani madhubuti kiuchumi.

Mafunzo rejea hayo kwa maofisa ugani wa serikali ni matunda ya ushirikiano kati ya serikali kupitia Wizara ya Kilimo na taasisi ya AMDT, ambayo kwa sasa imewekeza sana katika kuwezesha mapinduzi kwenye sekta ndogo za alizeti, mahindi na mazao jamii ya mikunde ikiwamo mbaazi. Sambamba na mafunzo haya yaliyotekelezwa katika halmashauri zote zinazolima alizeti nchini, Wizara na AMDT pia wamechapisha Mwongozo na Kalenda za Kilimo Bora cha Alizeti nchini. Majarida haya yatasambazwa katika mikoa yote inayozalisha zao hilo nchini kuanzia wiki ijayo.

Taasisi ya AMDT pia inashirikiana na wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya TARI, kituo cha Ilonga katika utafiti, uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za alizeti nchini. Mradi huu ni mwendelezo wa juhudi za pamoja kuboresha uzalishaji na uongezaji thamani wa alizeti, zao kubwa zaidi katika sekta ya mafuta ya kula nchini Tanzania.

Awamu hii ya mafunzo rejea ya maofisa ugani yamefanyika mikoa ya Tabora, Simiyu, Mara, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Dodoma, Morogoro na Njombe. Mingine ni Ruvuma, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa, Kigoma, Mtwara, Shinyanga na Lindi.

Mtendaji Mkuu wa AMDT, Charles Ogutu, alisema taasisi hii ni wakfu/mfuko maalum ulioanzishwa mwaka 2015 na serikali za Sweden, Denmark, Ireland na Uswisi kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo moja kuu; kuleta mapinduzi makubwa kwenye kilimo kwa kuboresha mifumo ya masoko ya sekta zetu za kilimo.

"Tumewekeza kwenye hili kwa miaka sita hivi tukifikia mikoa 24 ya Tanzania. Na bado tunataka kufika mbali zaidi," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo (katikati), akifanya uzinduzi wa tuzo za viwanda kwa wanawake Tanzania 2022 jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Mercy Sila, na (kushoto) ni Mkurugenzi wa chama hicho, Mwajuma Hamza. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vijana mazingira magumu wafundishwa kuanza miradi

**Na Francis Godwin,** IRINGA

VIJANA wanaotoka katika mazingira magumu kata za Ihanu, Luhunga na Mdabulo, Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, wameanza kupatiwa mafunzo maalumu ya uanzishaji miradi ya kiuchumi itakayowawezesha kuendesha maisha yao na kusaidia familia zao.

Mafunzo hayo ya siku 10 yameanza jana katika ukumbi wa Yatima Kijiji cha Igoda, Wilaya ya Mufindi kwa kushirikisha vijana hao ambao baadhi yao wamekatisha masomo kwa changamoto mbalimbali kimaisha ikiwa ni pamoja na mabinti kupata ujauzito.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, John Kalolo, kutoka Shirika lisilo la kiserikali la RLABS -Tanzania, alisema mafunzo hayo maalum ni ya kuwajengea uwezo katika nyanja ya ujasiriamali yatawezesha vijana hao kuondokana na fikra mgando kuwa ili uwe mjasiriamali ni lazima kuwa na fedha mkononi wakati unaweza kuanza bila mtaji wa fedha.

"Maeneo mengi ya vijijini kuna fursa nyingi za kufanya ambazo kimsingi ni moja kati ya mtaji mkubwa kwa mtu ambaye anatamani kuwa mjasiriamali hivyo iwapo wahusika wataondokana na fikra mgando za kutegemea fedha, wanaweza kupiga hatua katika maisha," alisema.

Vilevile, alisema ili vijana hao waweze kuondokana na dhana hiyo potofu ni lazima kwanza wajitambue na kujiamini kabla ya kuanza shughuli ya ujasiriamali ambayo anahitaji kuifanya na baada ya kuanza ndipo wanaweza kuanza mchakato wa pili wa kuomba mikopo ya kuboresha shughuli husika.

Hata hivyo, alisema kupitia ardhi walizonazo vijijini ziwe za familia ama zao binafsi wanaweza kubuni miradi ya kiuchumi ambayo anahitaji mtaji mkubwa wa fedha zaidi ya nguvu kazi ya mkono.

Kalolo alitoa mfano wa ujasiriamali wa ususi ambao mtu anaweza kuanza kwa ubunifu usiotegemea fedha na baada ya kuanza wanaweza kuboresha kwa kutafuta eneo litakalohitaji fedha za kuboresha zaidi.

Akizungumzia faida ya mafunzo hayo, meneja wa mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM) Zilipa alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha vijana zaidi ya 770 wakiwamo watoto 150 yatima kutoka kata hizo tatu ambazo zote zitaunganishwa na vijiji 16 za mradi huo.

Alisema mradi huo ni wa miaka minne toka mwaka 2021/2024 umefadhiliwa na Serikali ya Finland chini ya taasisi yake ya Diaconess kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na taasisi ya Foxes Community and Wild Life Conservation.

Mgeni alisema baada ya mafunzo hayo walengwa watawezeshwa mitaji ya kuendeshea miradi ambayo watakuwa wamechagua kuifanya kwa kuwaongezea nguvu ya kuiboresha zaidi.

Wilaya ya Mufindi ni moja kati ya tatu za mikoa wa Iringa zenye changamoto ya vijana na watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kupitia serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo wameendelea kuwawezesha vijana hao kuanzisha miradi ya kiuchumi inayowafanya kupiga hatua za kimaendeleo.

# Wateja M-Pesa kuvuna gawio la bil. 3.4/-

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya teknolojia na mawasiliano nchini, Vodacom Tanzania PLC imetangaza kuwa itatoa Sh. bilioni 3.4 ikiwa ni gawio kwa wateja wake wa M-Pesa ambao wametumia huduma hiyo robo ya nne ya mwaka huu (Oktoba hadi Desemba).

Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, alisema jana kuwa faida italipwa kwa wateja wote, mawakala wa rejareja na washirika wengine wa biashara wa M-Pesa ambao watapokea malipo kutokana na huduma ya malipo waliyofanya kupitia simu zao za mkononi.

"Huduma yetu ya pesa kupitia simu za mkononi, M-Pesa, inaendelea kuwa hadithi ya mafanikio ya kushangaza, ikitoa thamani kubwa ya kijamii na kifedha kwa Watanzania. Tumeona ukuaji mkubwa kwenye jukwaa la M-Pesa na wateja zaidi, mawakala, wafanyabiashara na taasisi zinazofanya biashara kufikia karibu shilingi bilioni 100 kila siku. Leo tunayo furaha kushiriki katika utoaji wa gawio la Sh. bilioni 3.4 kwa wateja wetu wapatao milioni 8 kote nchini," alisema.

Vodacom Tanzania PLC ina zaidi ya wateja milioni 11 kwenye jukwaa lake la M-Pesa inayomiliki sehemu ya soko ya asilimia 40 kulingana na takwimu za TCRA za hivi karibuni. Hadi sasa kampuni imelipa zaidi ya shilingi bilioni 171 ikiwa ni riba iliyolipwa tangu Julai 2015 Benki Kuu ya Tanzania (BoT) i ilipotunga kanuni hiyo.

Mbeteni aliongeza kuwa sehemu ya faida kwa kila mteja imehesabiwa kulingana na namna mteja alivyotumia huduma ya M-Pesa pamoja na mambo mengine, kiwango cha shughuli ambazo wamezifanya kupitia M-Pesa kwa kipindi hicho.

# Serikali yakunwa kozi ya urubani NIT

**Na Prosper Makene**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, amekipongeza Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuanza kutoa kozi za urubani kabla ya kumalizika kwa mwaka huu.

Katika kuanza kutoa kozi hizo za urubani, Benki ya Dunia imekipatia chuo hicho Sh. 48.9 bilioni kwa ajili ya ununuzi wa ndege tatu za mafunzo, kujenga karakana, na hosteli.

Akizungumza baada ya kutembelea chuo hicho katika ziara yake tangu kuteuliwa kushika wadhifa huo, alisema kabla ya kuanza kutolewa kwa kozi hizo, Watanzania walikuwa wakienda nje ya nchi kama Afrika

Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema wapo katika hatua za mwisho mwisho na wanatarajia kabla ya kuisha kwa mwaka huu wa 2022 wataanza kufundisha kozi ya urubani wa ndege.

HABARI KITAIFA

# Msajili Hazina aipa siri Posta kupaa kimapato

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MSAJILI wa Hazina, Mgonya Benedicto, amelitaka Shirika la Posta Tanzania kuwa na ubunifu katika kutekeleza majukumu yao ya kisheria ili kuongeza mapato na kutoa gawiwo stahiki katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Benedicto aliyasema hayo jana alipokuwa akifunga mkutano wa 28 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika hilo uliofanyika jijini hapa.

"Nafikiri mtaelewa Msajili wa Hazina anaposimama kitu cha kwanza anaangalia gawio katika taasisi zake na ndio maana mara nyingi huwa nahimiza shirika au kampuni wawe na ufanisi kwenye utekelezaji wao wa majukumu," alisema.

Aidha, alitaka shirika hilo kutumia kwa weledi fedha zilizotolewa na serikali ili kukidhi matarajio yake.

Alibainisha kuwa mwaka jana serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iliamua kuchukua jukumu la kuwalipa wastaafu wa liliyokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki na kurejesha kiasi chote cha Sh. bilioni 7.9 ambacho kilikuwa hakijarejeshwa.

"Serikali ilifanya maamuzi haya ili kuweka mazingira wezeshi kwa shirika kuongeza uzalishaji na kutekeleza majukumu yake ili kuendana na lengo la uanzishaji wa shirika na kwa mujibu wa sheria iliyounda shirika.

Kwa kuwa serikali ilifanya maamuzi haya ili kuongeza uzalishaji na kujipambanua katika utendaji wake napenda kuwasihi na kuelekeza kutumia fedha hizo kwa weledi ili kutimiza azma hiyo ya serikali na muende mbali zaidi ya mategemeo," alisema.

Msajili huyo alisema ofisi yake itaendelea kushirikiana na shirika katika utatuzi wa kero za kiuendeshaji na kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa kushirikiana na serikali ikiwamo suala la mtaji wa shirika na malimbikizo ya madeni ya kodi ya muda mrefu.

"Kwenye madeni ya kodi ya muda mrefu ni taribani Sh. bilioni 26 yanatakiwa kuchukuliwa na serikali," alisema.

Awali, Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika hilo, Macrice Mbodo, alisema wajumbe wa baraza hilo wamepatiwa mafunzo mbalimbali ikiwamo ya kujengewa uwezo wa kiuongozi bila kusukumana wala kusigana.



Mkuu wa Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC), Aristid Kanje (kulia), akifafanua jambo kwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete (wapili kushoto), kuhusu mipango ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kujenga madarasa, wakati alipotembelea eneo lililotengwa kwa ajili ya kujenga madarasa hayo jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: DICKSON MULASHANI**

# MTAKUWWA ilivyofanikiwa kupunguza ukatili kijinsia

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

KAMATI ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), Kata ya Puni Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, imesaidia kupunguza vitendo vya kikatili wanavyofanyiwa watoto wa kike na wanafunzi.

Wajumbe wa kamati hiyo walizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti jana, wakati wa utekelezaji wa mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, unatokelezwa na SPC kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mmoja wa wajumbe hao Damson Fofo alisema, kabla ya kuundwa kwa kamati hiyo kulikuwa na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia na asilimia kubwa ya waathirika walikuwa kinamama na watoto wa jinsi ya kike kupelekwa kwa waganga wa jadi kuogeshwa dawa za mvuto wa mapenzi.

Alisema, wazazi wengi walikuwa wakiyafanya hayo ili kuepukana na mimba za ututoni kwa mabinti zao bila kutambua pia kumwozesha mtoto akiwa na umri wa chini ya miaka 18 ni ukatili na baada ya kundwa kwa kamati hiyo matukio ya ukatili yamepungua.

Naye Lucy Michael, alisema wamekuwa wakikutana kila baada ya miezi mitatu na kwa mwaka mmoja wanakutana mara nne lengo likiwa ni kukumbushana wajibu na kuendelea kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wananchi walioko pembezoni mwa kata ili watambue wapi wanatakiwa kuanza kutoa taarifa.

Michael alisema, siku ya magulio na minada wajumbe wanafika na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia na kuwasihi wazazi kuongozana na watoto wao siku hizo ili wanaume au vijana wanaowarubuni watoto wao hasa wanafunzi wakose nafasi na kumpatia nafasi mtoto kuendelea na masomo.

"Utoaji wa elimu ya ukatili wa kijinsia mara kwa mara kwa wananchi wetu umesaidia kuwafungua upeo na wamekuwa wakitoa taarifa pale wanapoona viashiria vya ukatili ndani ya familia, mimba, ndoa za ututoni, baba kutelekeza familia zimepungua kwa sasa," alisema Michael.

Kwa upande wake Katibu wa MTAKUWWA, ambaye ni Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Puni, Rebeca Ruwa, alisema kabla ya kamati hiyo hali ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ilikuwa mbaya zaidi na kwa siku moja alikuwa akipokea matukio matano na wakati mwingine 10.

Alisema, matukio yaliyokuwa yakiripotiwa mara kwa mara ilikuwa kupigwa kwa wanawake ndani ya familia na waume zao na watoto wa kike hasa wanafunzi kuzuiliwa kwenda shule kwa lengo la kutaka kuozeshwa baada ya mzazi kuchukua mahari ya ng'ombe wawapo kwenye vilabu vya pombe.

Vile vile, alisema kwa sasa vitendo hivyo vimepungua na kwa siku yanaripotiwa matukio mawili na wakati mwingine hakuna kwasababu ya elimu inayoendelea kutolewa mara kwa mara kwa wananchi na kuwataka kutoa taarifa za vitendo vya kikatili ambavyo vinatokea ndani ya familia.

## TASAF yawezesha wanafunzi sare

**Na Elizabeth Zaya**

MPANGO wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), umesaidia kuwezesha wanafunzi sare za shule na kuhudhuria shuleni.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwamsundi, Mkata wilayani Handeni, Hosen Mkangara, alisema wanafunzi wengi katika kijiji hicho walikuwa wanashindwa kwenda shuleni kwa kukosa sare za shule.

Alisema tatizo hilo lilichangiwa na wazazi wengi wa kijiji hicho kukabiliwa na umaskini na hivyo kushindwa kumudu kuwanunulia watoto wa sare hizo za shule.

Alisema hata wanafunzi wachache waliokuwa na shauku kubwa ya kusoma walijikuta wakienda na nguo za kawaida na hivyo kuwapa wakati mgumu walimu.

"Hapa kwetu ilikuwa ni jambo la kawaida kuona wanafunzi wakijifunga kanga na kwenda shuleni hasa wale wa kike ambao walikuwa na shauku ya kusoma," alisema Mkangara.

## Faida ya EABL yapaa kwa 131 %

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Afrika (EABL) ambayo inamiliki asilimia kubwa ya hisa katika kampuni ya Bia ya Serengeti, imeripoti mauzo yanayofikia fedha za Kenya shilingi bilioni 54. 9, ambazo ni zaidi ya shilingi za Kitanzania trilioni moja katika kipindi kinochoishia mwezi Desemba 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia 23 ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka uliopita.

EABL inamiliki kampuni kubwa tatu za bia katika ukanda wa Afrika Mashariki ikiwamo Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) Kampuni ya Bia ya Kenya (KBL) na Kampuni ya Bia ya Uganda (UBL)

Ukuaji wa asilimia 23 umewezeshwa na uwekezaji pamoja na uvumbuzi ambao umekuwa ukifanyika kwenye bidhaa mbalimbali za kampuni za EABL ukienda sambamba na kufuata mahitaji na tabia za wateja ambazo zimekuwa zikibadilika mara kwa mara.

Kampuni hiyo pia imeendelea kuwekeza kwenye upanuzi wa biashara zake. Uwekezaji wa shilingi za Kenya bilioni 6.2 sawa na zaidi bilioni shilingi za Kitanzania bilio 122 umefanyika. Faida baada ya kodi imekuwa kwa asilimia 131 na kufikia fedha za kenya shilingi bilioni 8.7 sawa na fedha Tanzania zaidi ya shilingi bilioni 175.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA MABAO 100 HARAKA ZAIDI UK. 12 - 13



MESSI

RONALDO

# WANASOKA WATANO MATAJIRI ZAIDI 2022

## ISIKUPITE

REKODI ya mchezaji ghali mwenye umri chini ya miaka 18, inashikiliwa na mshambuliaji wa Real Madrid, Vinicius Jr ambaye alinunuliwa kwa kiasi cha euro milioni 45, Rodrygo (euro milioni 45), Fabio Silva (euro milioni 40), Luke Shaw (euro milioni 37.5) na Wayne Rooney (euro milioni 37).



**LONDON,** Uingereza

SOKA ndio mchezo maarufu zaidi duniani. Hakika ni mchezo unaofuatiliwa zaidi kwenye sayari hii. Kutokana na mvuto wake wa kimataifa, kuna fedha nyingi zinazohusika na mchezo huo. Timu za soka na wanasoka wanasherehekea kila mahali na hii hutafsiri kwa kiasi cha ajabu cha mapato wanayoyapata.

Wanasoka ni baadhi ya wanamichezo maarufu duniani. Kwa sababu ya ukweli kwamba wengi wao wamekuwa na majina makubwa kote ulimwenguni.

Si hivyo tu, wanasoka wakubwa pia wanapata mikataba minono na klabu tajiri zaidi duniani. Pia wanakuwa na mahusiano ya kimikataba na makampuni mbalimbali ya uwekezaji wa hali ya juu, ambayo yanawasaidia kuishi maisha ya anasa. Hebu sasa tuwaangalie wanasoka watano matajiri zaidi duniani kwa mwaka 2022...

### #5. ALEXANDRE PATO (DOLA MIL. 145)

Ndani ya dimba, Alexandre Pato hana mafanikio makubwa sana ya kiuchezeshaji. Baada ya yote, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kwa sasa, anachezea klabu ya Orlando City ya nchini Marekani. Na anaukwasi wa kutosha.

Nje ya uwanja, Pato amefanya vyema. Kwa kweli, yeye ni mmoja wa wanasoka matajiri zaidi kwenye sayari hii. Nafasi pekee nzuri ya Pato akiwa na klabu kubwa ilikuwa AC Milan. Hata huko, kukaa kwake kulikumbwa na masaibu ya majeraha.

Lakini Mbrazil huyo ana utajiri wa dola milioni 145, ambazo ni zaidi ya Wayne Rooney, Gareth Bale, Eden Hazard, Zlatan Ibrahimovic na Ronaldinho.

Utajiri wa ajabu wa Pato umeripotiwa kuwa unatokana na uwekezaji mzuri, umiliki wa mali kubwa na dili la faida kubwa la vipodozi vya CoverGirl. Yeye pia ni mmiliki wa msururu wa migahawa ya baga nchini Brazili inayoitwa 'Fat Pato Burger', mtindo unaoitwa 'Alexandre Pato Seduction' na lebo ya vodka iitwayo 'Wonderpato - Brazil'.

### #4. DAVE WHELAN (DOLA MIL. 220)

Mwanasoka wa zamani wa England na mfanyabiashara Dave Whelan alikuwa mmoja wa watu matajiri zaidi kuwahi kucheza mchezo huo kutokana na kile alichokifanya mara tu alipotundika daluga zake.

Whelan aliichezea Blackburn Rovers na Crewe Alexandra wakati wa uchezaji wake kati ya mwaka 1956-1966. Muda mfupi baada ya kustaafu, alifungua maduka makubwa kadhaa yaitwayo 'Whelan's Discount Stores'.

Baadaye alinunua duka la michezo na uvuvi lililoitwa JJB na kuligeuza kuwa muuzaji wa pili kwa ukubwa nchini Uingereza. Aliuza hisa zake katika kampuni hiyo mwaka wa 2007. Whelan anajulikana zaidi kwa muda wake kama mmiliki wa Wigan Athletic, baada ya kuinunua klabu hiyo mwaka 1995.

### #3. LIONEL MESSI (DOLA MIL. 400)

Unapokuwa mwanasoka bora zaidi wa wakati wote, unakuwa mmoja wa watu wanaotambulika zaidi kwenye sayari hii. Hii ni dhahiri inakufanya upate mikataba yenye faida kubwa. Lionel Messi ameshinda Ballon d'Or mara saba ikiwa ni rekodi. Tuzo hii ni ya mchezaji binafsi yenye hadhi kubwa zaidi katika soka.

Anaripotiwa kuwa mchezaji wa soka anayelipwa zaidi katika suala la mshahara. Kwa mujibu wa Forbes, Messi anapata hadi dola milioni 165 kila mwaka kama mshahara na motisha. Raia huyo wa Argentina alianzisha lebo ya nguo zake na akafungua 'Duka la Messi', mwaka 2019.

Messi pia amesaini mkataba wa maisha na Kampuni ya Adidas. Akiwa Paris Saint-Germain, Messi anaripotiwa kupokea takriban milioni moja kwa wiki. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, anapendwa kote duniani na inashangaza kwamba yeye si mwanasoka namba moja kwa utajiri duniani.

### #2. DAVID BECKHAM (DOLA MIL. 450)

Je, kuna uso unaotambulika zaidi kutoka kwa ulimwengu wa soka kuliko David Beckham? Alikuwa mwanasoka wa aina yake wa England na akashinda mataji ya ligi kwenye nchi nne tofauti. Umaarufu wake mkubwa ulitokana na uwezo wake wa ajabu wa kiufundi na pia sura yake nzuri.

Beckham alikuwa mchezaji mwenye soko kubwa zaidi miaka ya 2000. Alikuwa mmoja wa wapiga mpira wa adhabu ndogo bora zaidi, alikuwa na haiba ya kupendeza na alichezea baadhi ya klabu kubwa duniani. Ana uwekezaji katika sekta mbalimbali kama vile chakula na vinywaji, mitindo, televisheni na burudani.

Pia yeye ni mmiliki mwenza wa klabu ya Ligi Kuu ya Marakeni, Inter Miami. Beckham ana mkataba mzuri wa kuidhinisha na muuzaji wa rejareja wa H&M. Saa za Tudor, whisky ya Haig Club, Breitling, Sainsbury's, Armani, Gillette, AIA Group, Adidas na Pepsi Co. Zote ni bidhaa kubwa ambazo ameshirikiana nazo.

### #1. CRISTIANO RONALDO (DOLA MIL 450)

Bado mchezaji mwingine ambaye yuko kwenye kinyang'anyiro cha mwanasoka bora wa wakati wote, Cristiano Ronaldo, ni mmoja wa wanamichezo maarufu zaidi kwenye sayari. Ronaldo ni mashine na hata akiwa na umri wa miaka 36, anaendelea kuwa mmoja wa wanasoka bora zaidi duniani.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, ameshinda mataji ya ligi katika nchi tatu tofauti. Alicheza kwa kuvunja rekodi akiwa na Real Madrid na Juventus na amerejea Manchester United kwa kipindi cha pili. Mbali na kuwa mmoja wa wanamichezo bora duniani, Ronaldo pia ameonyesha kuwa ni mjasiriamali mkubwa.

Amefungua kliniki za upandikizaji wa nywele Hispania na Ureno zinazoitwa 'Insparya'. Ronaldo ana mkataba mnono na Nike na ameshirikiana na kampuni kadhaa maarufu kama Herbalife, Armani, Clear Shampoo na Unilever, ukitaja kwa chache. Pia ana lebo ya hoteli ya kifahari iitwayo 'CR7' kwa ushirikiano na Pestana Group. Hoteli hizi zipo Ureno, Marekani na Hispania.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ndiye mwanasoka tajiri zaidi duniani kwa sasa.

# WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA MABAO 100 HARAKA ZAIDI

**LONDON,** England

MCHEZO wa soka umepambwa na wafungaji wengi mahiri kwa miaka mingi, haswa tangu mwanzo wa karne hii. Baadhi ya wachezaji hao bado wanaendelea vema licha ya umri wao kugonga zaidi ya miaka 30.

**Wachezaji kama Ronaldo Nazario, Ruud van Nistelrooy na hivi karibuni zaidi Robert Lewandowski, Cristiano Ronaldo, Lionel Messi na Luis Suarez, wamefunga mabao mengi.**

Wengi wa washambuliaji hawa wamefunga zaidi ya mabao 100 kwa klabu moja. Katika makala haya, hapa tunawaangalia wachezaji 10 ambao wamefunga mabao 100 kwa haraka katika klabu moja:

### #10. CIRO IMMOBILE (LAZIO) – MECHI 147 (2019)

Tofauti na wachezaji wengi kwenye orodha hii, Ciro Immobile amechelewa kung'ara. Baada ya kujiunga na Lazio mwanzoni mwa msimu wa 2016-17, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, tayari amepachika zaidi ya mabao 170 kwenye mashindano yote. Hilo likamfanya kuwa mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo yenye makao yake makuu jijini Roma.

Immobile ameshinda tuzo mbili kati ya tatu za Capocannoniere (mfungaji bora) akiwa na Lazio. Msimu wa 2019-20, alifunga mabao 36 kwenye ligi na kufikia rekodi ya Gonzalo Higuain ya kufunga mabao mengi zaidi katika msimu mmoja wa Serie A.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia, amefikisha mabao 172 kwenye Serie A, huku mabao yake mengi (140) akiifungia Lazio. Msimu huu, tayari amefikisha mabao 17 huku akiwa kwenye nafasi ya kuwania tuzo yake ya nne ya Capocannonieri.

### #9. CHRISTIAN VIERI (INTER MILAN) – MECHI 138 (2004)

Christian Vieri alikuwa mfungaji hodari wa klabu na nchi. Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Italia alichezea zaidi ya klabu kumi tofauti, haswa nchini Italia, lakini alifurahia kipindi chake kizuri zaidi akiwa na Inter Milan.

Katika kipindi cha miaka sita akiwa na Nerazzurri hao mwishoni mwa miaka ya 90 na mwanzoni mwa miaka ya 2000, nyota huyo mwenye umri wa miaka 48, alifunga mabao 123 katika takriban michezo 200 kwenye mashindano yote. Vieri alifunga mabao 24 ya ligi kwa msimu wa 2002-03 na kushinda tuzo yake pekee ya Capocannonieri (mfungaji bora).

Inter ililazimika kulipa ada ya rekodi ya Dunia wakati huo ya pauni milioni 28 kukamilisha uhamisho huo ambao ulimfanya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Italia kuungana na Ronaldo katika safu ya ushambuliaji. Kwa uhamisho huu Vieri alikuwa katika 10 bora ya uhamisho ghali zaidi wa wakati wote mara tatu.

Hakuweza kushinda ligi akiwa na Inter, lakini alishinda taji lake pekee la Serie A akiwa na Juventus msimu wa 1996-97.

### #8. KYLIAN MBAPPE (PSG) - MECHI 137 (2020)

Kylian Mbappe anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi vijana kwa sasa.

Akiwa na umri wa miaka 23 tu, Mfaransa huyo tayari ana mataji mengi kwenye kabati lake, ameshinda mataji mengi makubwa akiwa na klabu na nchi. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018, amekuwa mchezaji bora wa Paris Saint-Germain (PSG). Amefunga mabao 151 na asisti 92 katika michezo 204 katika mashindano yote kwa klabu hiyo.

Mbappe hivi majuzi alifikisha mabao 150 kwa PSG, na kuwa mchezaji wa tatu kufanya hivyo pale Les Parisiens.

Baada ya mabao 42 msimu wa 2020-2021, Mbappe amefikisha mabao 22 msimu wa sasa unaoendelea na pia ametengeneza asisti 18 akiwazidi Lionel Messi na Neymar.

### #7. ROBERT LEWANDOWSKI (BAYERN MUNICH) – MECHI 136 (2017)

Robert Lewandowski ni mashine ya mabao. Tangu ajiunge na Bayern Munich kwa uhamisho huru msimu wa majira ya joto wa mwaka 2014, mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland amefunga mabao 328 katika mashindano yote akiwa na wababe hao wa Bavaria.

Msimu uliopita, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alifunga mabao 41 akivunja rekodi ya Gerd Muller aliyefunga 40 kwa msimu, rekodi iliyokaa kwa zaidi ya miongo mitano katika Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga. Msimu huu pia amekuwa wa moto kwani tayari amefikisha mabao 34 katika mashindano yote, huku 23 kati yao yakiwa kwenye ligi.

Lewandowski sasa ameifungia Bayern Munich mabao 300 katika michezo 333. Pia amechangia kwa asisti 65. Hivi sasa Lewandowski amejiunga na marehemu Muller kama mchezaji pekee aliyefunga mabao 300 kwenye Bundesliga.

### #6. EDINSON CAVANI (PSG) - MECHI 135 (2015)

Edinson Cavani ni mmoja wa washambuliaji mahiri katika mchezo huo. Raia huyo wa Uruguay, ambaye sasa anakipiga katika klabu ya Manchester United, amefunga mabao mengi katika ligi nyingi.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Napoli na Palermo alifurahia kipindi chake kitamu akiwa na PSG, ambapo aliifungia mabao 200 katika misimu saba. Mfungaji huyo bora wa muda wote wa klabu hiyo alishinda mataji sita ya ligi akiwa na wababe hao wa Ligue 1.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alifurahia msimu bora wa 2016-17, na akitikisa nyavu mara 49, yakiwamo 35 ya ligi. Cavani pia aliifungia Napoli mabao 104.



RONALDO

### #5. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS) - MECHI 131 (2021)

Cristiano Ronaldo anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi waliowahi kuupamba mchezo huo mzuri.

Mfungaji bora wa mabao, mwenye umri wa miaka 36, amefurahia mafanikio makubwa katika klabu nyingi na katika nchi nyingi. Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or, ambaye sasa amerejea Manchester United, alifurahia uchezaji mzuri wa misimu mitatu akiwa na wababe hao wa Italia, Juventus.

Ingawa hakuweza kumaliza ukame wao wa karibu wa miongo mitatu wa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ronaldo alifunga mabao mengi kwa 'Bianconeri' hao. Katika msimu wake wa tatu na wa mwisho akiwa nao, 2020-21, alikuwa mchezaji aliyefunga mabao 100 kwa haraka zaidi kwenye historia ya klabu hiyo.

Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza kushinda kila taji la ndani katika ligi tatu kati ya tano bora za Ulaya na kuwa mfungaji bora katika historia ya soka la kimataifa.

### #4. RUUD VAN NISTELROOY (MANCHESTER UNITED) - MECHI 131 (2004)

Ruud van Nistelrooy alikuwa mfungaji mabao hatari wakati wa enzi zake za uchezaji. Nistelrooy mwenye umri wa miaka 45, alifurahia maisha mazuri akiwa na wababe wa England, Manchester United mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Van Nistelrooy alifunga mabao 150 kwa 'Mashetani Wekundu' hao ndani ya misimu mitano pekee. Cha kufurahisha ni kwamba mabao yake yote isipokuwa moja ya klabu yalitoka ndani ya eneo la hatari. Lakini raia huyo wa Uholanzi alikuwa na taji moja tu la Ligi Kuu England.

Van Nistelrooy baadaye aliendelea kufurahia soka akiwa Real Madrid ambako alifunga mabao 64 katika misimu minne na kushinda mataji mawili ya ligi.

### #3. ZLATAN IBRAHIMOVIC (PSG) - MECHI 124 (2015)

Zlatan Ibrahimovic ni mmoja wa wafungaji bora wa mchezo huo, haswa tangu mwanzoni mwa karne hii.

Akiwa bado na nguvu kwa umri wake wa miaka 40, Msweden huyo amefunga mabao na kushinda mataji ya ligi katika nchi nne tofauti. Hivi majuzi Ibrahimovic alifunga bao lake la 150 kwenye Serie A, ambalo pia lilikuwa bao lake la 400 katika soka kwenye ligi.

Akiwa amezichezea klabu za Juventus, Barcelona na Manchester United, mshambuliaji huyo wa AC Milan alifurahia maisha mazuri akiwa na PSG. Katika misimu minne kule Paris, alifunga zaidi ya mabao 150 na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo.

Baadaye alizidiwa na Cavani, wakati Mbappe pia yuko mbioni kuifikia idadi hiyo ya mabao ya Msweden huyo kwa wababe hao wa Ligue 1.

### #2. LUIS SUAREZ (BARCELONA) - MECHI 120 (2017)

Luis Suarez ni mfungaji mwingine mwenye uwezo mkubwa wa kufunga mabao. Ingawa inaeleweka uwezo wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 unazidi kupungua, amefunga mabao mengi kwa klabu kubwa.

Raia huyo wa Uruguay alifurahia maisha mazuri akiwa na Barcelona, akifunga takriban mabao 200 katika misimu sita kwenye klabu hiyo. Msimu wa 2015-16, alifunga mabao 40 ya ligi, akiwazidi Cristiano Ronaldo na Lionel Messi kama mchezaji pekee aliyefanya hivyo katika historia ya LaLiga. Alishinda tuzo mbili za 'Kiatu cha Dhahabu' cha Ulaya.

Mshindi huyo mara tano wa taji la LaLiga, kwa sasa yuko na Atletico Madrid, ambayo ameifungia mara 30 katika michezo 68 kwenye mashindano yote.

### #1. CRISTIANO RONALDO (REAL MADRID) - MECHI 105 (2011)

Cristiano Ronaldo ndiye mchezaji pekee kwenye orodha hii ambaye ametokea mara mbili, na kwa sababu nzuri tu.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, amefunga mabao kila mahali alipocheza, lakini alifurahia maisha mazuri zaidi akiwa na Real Madrid. Ronaldo alifunga mabao 450 katika mechi 438 kwa misimu tisa akiwa na 'Los Blancos' hao.

Kwa sasa akiwa Manchester United, mshindi huyo mara tano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya amefunga zaidi ya mabao 800 kwa klabu na nchi. Akiwa na mabao 115 kwa Ureno, pia ndiye mfungaji bora zaidi katika soka la kimataifa kwa wanaume.

## Nukuu



"Sikuwa na hofu kutumia mbinu ya namba tisa wa uongo/wakuibia (false nine) kwa sababu Uwanja wa Kaitaba unaruhusu kutengeneza nafasi nyingi za kufunga. Nakiri bado washambuliaji wangu hawajawa sawa, ila ni kawaida kwa washambuliaji kupitia nyakati ngumu. Naendelea kufanya kazi ya ziada ili kuwarejesha kwenye makali yao," **Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Fraco baada ya kupoteza dhidi ya Kagera Sugar**



"Nadhani N'Golo sasa yuko bega kwa bega na kiungo yeyote wa kati wa klabu hii. Unaweza kumweka karibu na Frank [Lampard], unaweza kumweka karibu na [Claude] Makelele. Ikiwa ataendelea miaka michache zaidi na kupata mafanikio zaidi labda atawazidi. Katika suala la ushawishi uwanjani, sidhani kama kuna kiungo mwenye ushawishi mkubwa katika soka la dunia, asipocheza inatuumiza sana. Yeye ndiye mchezaji pekee kwenye kikosi ukimtoa nje ni vigumu kupata mbadala wake," **Nyota wa zamani wa Chelsea, Joe Cole akielezea makubwa kuhusu kiungo N'Golo Kante wa klabu hiyo.**



"Paris, tuna wachezaji wengi ambao wanaweza kupiga 'mipira iliyokufa' (free kicks). Kuna Messi [Lionel], Neymar, Mbappe [Kylian], ninajaribu, lakini ni vigumu. Nitazungumza nao wakati nitakaporudi Paris. Kwa sasa ninaangazia timu ya taifa, lakini baadaye, tutaona kitakachotokea Paris," **beki wa PSG, Achraf Hakimi, baada ya kuifungia Morocco bao la ushindi kwa free kicks dhidi ya Malawi wakati wakishinda 2-1 na kutinga 16-bora kwenye Afcon.**

TANGAZO

Access Microfinance Bank Tanzania

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa<br>31 DISEMBA 2021 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita)<br>31 DISEMBA 2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa<br>31 DISEMBA 2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita)<br>31 DISEMBA 2020 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 4,331 | 3,775 | 16,053 | 15,092 |
| 2 Gharama za Riba | (570) | (727) | (2,506) | (4,443) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | 3,761 | 3,048 | 13,547 | 10,649 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (229) | (859) | (1,712) | (2,460) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **925** | **721** | **3,448** | **2,818** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 54 | 110 | 162 | 279 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 277 | 255 | 1,006 | 1,150 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 594 | 356 | 2,280 | 1,389 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(4,708)** | **(4,328)** | **(15,825)** | **(22,153)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,817) | (1,957) | (9,123) | (11,232) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (134) | (268) | (584) | (1,007) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (1,757) | (2,103) | (6,119) | (9,914) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(249)** | **(1,418)** | **(542)** | **(11,146)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | 3,344 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(249)** | **(1,418)** | **(542)** | **(7,802)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | 426 | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(249)** | **(992)** | **(542)** | **(7,802)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 341 | 306 | 341 | 306 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (25) | (99) | (14) | (260) |
| 15 Idadi ya Matawi | 8 | 8 | 8 | 8 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.7% | -4.5% | -0.9% | -7.9% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -14.9% | -28.6% | -8.0% | -36.3% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 89.6% | 96.3% | 81.2% | 123.7% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 39.6% | 30.7% | 34.8% | 22.1% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa<br>31 DISEMBA 2021 | Robo Mwaka iliyopita<br>30 SEPTEMBA 2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa<br>31 DISEMBA 2021 | Limbikizo la robo Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita)<br>31 DISEMBA 202 |
|---|---|---|---|---|
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (249) | 170 | (542) | (11,146 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 499 | 639 | 2,731 | 4,017 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,234) | (900) | (2,715) | 23,290 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (35) | (7) | (42) | 11 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,251) | 901 | (6,677) | (26,626 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (35) | 136 | 919 | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (16) | (158) | (4,634) | (2,722 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 987 | (1,019) | 1,943 | (1,368 |
| - Kodi Iliyolipwa | (20) | (20) | (80) | (93) |
| - Mengineyo (bainisha) | (67) | 8 | 123 | 2,429 |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(1,422)** | **(250)** | **(8,975)** | **(12,210** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (18) | - | (18) | (35) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 41 | 9 | 60 | 13 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato ahirishwa | (39) | (48) | (145) | (118 |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(16)** | **(39)** | **(103)** | **(140** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | - | - | - | - |
| | | | - | - |
| **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(1,438)** | **(290)** | **(9,079)** | **(12,350** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **11,849** | **12,139** | **19,490** | **31,840** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Kipindi | **10,411** | **11,849** | **10,411** | **19,490** |




## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | (Kiasi kwa shilingi milioni) Robo Mwaka ya sasa<br>31 DISEMBA 2021 | Robo Mwaka iliopita<br>30 SEPTEMBA 2021 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 5,210 | 5,608 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 6,397 | 5,351 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 477 | 442 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 60 | 21 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | 2,500 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 37,495 | 36,261 |
| 12 | Mali Nyingine | 8,782 | 9,726 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,101 | 1,129 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **59,522** | **61,038** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 42,713 | 43,964 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,900 | 1,487 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,650 | 1,626 |
| 27 | Dhima Nyingine | 6,662 | 7,115 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **52,925** | **64,192** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **6,597** | **6,846** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 40,000 | 40,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (33,549) | (33,551) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (543) | (293) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 689 | 691 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | ***JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA*** | **6,597** | **6,846** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 816 | 376 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,707 | 7,175 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 5,222 | 5,494 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 64 | 64 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.08% | 11.22% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 15.70% | 17.18% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 100.01% | 94.98% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 62.99% | 59.41% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 62.99% | 63.50% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -2.85% | 2.09% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -2.48% | 1.52% |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipindi cha sasa hadi 31 Disemba 2021** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2021 | 40,000 | - | (35,570) | 2,709 | - | 7,139 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (543) | - | - | (543) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 2,020 | (2,020) | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2021** | **40,000** | **-** | **(34,092)** | **689** | **-** | **6,597** |
| **Kipindi cha Mwaka uliopita hadi 31 Disemba 2020** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2020 | 40,000 | - | (13,883) | - | - | 26,117 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (18,978) | - | - | (18,978) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (2,709) | 2,709 | - | - |
| **Salio la mwisho wa 31 Disemba 2020** | **40,000** | **-** | **(35,570)** | **2,709** | **-** | **7,139** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2021**

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Julius Justine Ruwaichi | Offisa Mtendaji Mkuu | Imesainiwa | 25 Januari 2022 |
| Tajinder Singh Bhachu | Kaimu Mkuu wa Fedha | Imesainiwa | 25 Januari 2022 |
| Catherine Temu | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | Imesainiwa | 25 Januari 2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| **Jina** | **Cheo** | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Thomas Engelhardt | Mwenyekiti | Imesainiwa | 25 Januari 2022 |
| Johannes Mainhardt | Mkurugenzi | Imesainiwa | 25 Januari 2022 |







Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (kushoto), akishiriki kufanya usafi wa mazingira na wakazi wa mtaa wa Kikuyu Kusini jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Makandarasi wafundwa utekelezaji miradi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAKANDARASI wametakiwa kuzingatia mafunzo wanayopata kwa kuhakikisha wanayatumia kuboresha kazi zao wakati wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki mkoani Dodoma na Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Consolata Ngimbwa, wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi wazawa.

Alisema CRB imejitahidi kuandaa mafunzo mengi yakiwamo ya namna ya kuandaa mikataba, kujaza zabuni kielektroniki na namna ya kuwasilisha zabuni hivyo lazima makandarasi wayatumie kuongeza ubora wa kazi zao.

"Kuna mtu anachangia mada kwenye mkutano lakini akitoka hapo getini yote aliyojifunza anayaacha hapo sasa naomba tuyaishi haya tunayojifunza kwasababu ni kwa faida yetu sisi wenyewe kukuza biashara hii. Mwezi ujao kutakuwa na mafunzo ya menejimenti na kufanya kazi kwa ubia naomba mhudhurie mwongeze ujuzi," alisema.

Alisema ni vizuri kuwatumia wataalamu kwenye utekelezaji wa shughuli zao, lakini wanapaswa kutokuwa wategemezi kupita kiasi hivyo watumie mafunzo hayo kujiweka sawa na kuachana na utegemezi wa kujaza zabuni na kuendesha kampuni zao.

Alisema kazi za ujenzi ziko nyingi, lakini za ushindani badala ya kukaa na kulalamika kwamba hawapati kazi wayatumie mafunzo hayo kuongeza ujuzi hasa kwenye kujaza zabuni kielektroniki na kuweka bei ambayo ni halisia.

"Hakuna kazi nyingi kwamba kila mtu atapata, lakini zipo za ushindani na ili uweze kushindana kwenye soko hili ni lazima uwe na ujuzi mkubwa kwenye menejimenti, kujaza zabuni na kusimamia mikataba sasa ukisikia mafunzo njoo yana faida kubwa," alisema.

Alisema serikali imejitahidi kutangaza zabuni nyingi za miradi ya maji na ujenzi wa barabara hivyo makandarasi wa ndani watakaobahatika kuipata wanapaswa kuitekeleza kwa ufanisi mkubwa.

"Mkifanya vizuri mnajitengenezea njia yenu na ya wengine kuaminiwa ukifanya vibaya unatuharibia na sisi kuaminiwa. Biashara hii ya ukandarasi ni nzuri tu na ya heshima kwa hiyo hakikisheni mnalinda heshima ya kazi yetu kwa kufanyakazi nzuri," alisema.

# Maofisa afya watakiwa kuwapa elimu w/biashara

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAOFISA afya wa Jiji la Dodoma wameshauriwa kutoa elimu ya kitaalamu kwa wafanyabiashara itakayosaidia kuboresha biashara zao badala ya kuzifunga na kupiga faini.

Ushauri huo ulitolewa na ofisa afya wa Jiji la Dodoma, Abdalah Mahia, alipokuwa akizungumza na maofisa afya kwa ajili ya zoezi la ukaguzi na usafi wa mazingira litakalofanyika kwenye kata zote.

Mahia, alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma kupitia idara ya afya inafanya operesheni maalum ya kudumu kwenye maeneo ya kuuzia vyakula, vinywaji, nyumba za kulala wageni na kuishi ili kuhakikisha zinakuwa safi.

Alisema kuwa usafi huo ambao utakuwa wa kudumu ni pamoja na ukaguzi wa vyoo na vyombo vya usafiri ambavyo vitakaguliwa kwa ajili ya upulizaji wa dawa ya kuulia wadudu na uwekaji wa mitungi ya kuzimia moto.

Mahia alisema usafi huo utakuwa endelevu kwa mujibu wa sheria ya afya ya jamii ya mwaka 2009, kupitia operesheni hiyo amewataka mama na baba lishe,wenye nyumba za kulala wageni na kuishi kushirikiana na maafisa wa afya kwenye maeneo yao ili zoezi hilo liweze kufanikiwa.

"Ukaguzi huu ni endelevu na umezingatia Sheria ya Afya Jamii ya Mwaka 2009 na kanuni yake ya mwaka 2012 kifungu cha 36 ambacho kinatoa kanuni, taratibu na masharti kwa wauza vyakula na vinywaji.

"Niwaombe watoa huduma kwenye maeneo yao suala la kuvaa sare ni muhimu lizingatiwe hii ni pamoja na uwekaji wa chombo cha kuifadhia taka na kwa upande wa watoa huduma ya vyakula maji yanakuwa ya moto na chombo cha kunaiwa kinakuwa na sabuni," alisisitiza Mahia.

# Aweso akerwa watu kunywa maji na mifugo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, amesema hayuko tayari kuendelea kuona wananchi wanakunywa maji kwa kuchangia na mifugo wakati serikali tayari imetoa fedha za miradi ya maji kwa wakati.

Aweso alisema hayo hivi karibuni jijini hapa wakati akishuhudia utiaji saini wa mikataba ya ununuzi wa pampu za maji 301, zinazolenga kufungwa katika mikoa mbalimbali nchini.

Alisema akiwa waziri mwenye dhamana ya maji hatakuwa tayari kuendelea kuona wananchi wanakunywa maji kwa kuchangia na mifugo wakati serikali tayari imetoa fedha nyingi kwa ajili ya miradi ya maji.

"Hatutakuwa tayari kuona mwananchi anaendelea kunywa maji na punda ili hali fedha za miradi ya maji tumepata kwa wakati," alisema Aweso.

Alisema serikali ya awamu ya sita inalengo la kumtua mama ndoo kichwani kwa kuboresha miundombinu ya maji pamoja na kuanzisha vyanzo vipya vya maji.

"Niwaagize Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA), kuhakikisha kuwa miradi yote ya maji inakamilika kwa wakati lakini kwa wale wote wanaofanya miradi hii wakikamilisha walipwe kwa wakati asiyefanya kazi na asile," alisisitiza Aweso.

Aidha, alisema ili kuleta ufanisi katika miradi ya maji ambayo imetumia kiasi kikibwa cha fedha zilizotolewa katika awamu hii ya sita anapanga kuitisha kikao kati ya wizara hiyo na makandarasi wanaotekeleza miradi ya maji nchini.

"Mwanzoni mwa mwezi Februari mwaka huu tutafanya kikao na makandarasi wote kwa kuwa wao wana yao ya kutueleza katika changamoto zao lakini na sisi serikali tuna yetu ya kuwaeleza lengo likiwa ni kufanikisha kuwafikishia huduma watanzania wote katika maeneo yote," alisema.

Pia, aliwataka wazabuni wa miradi ya maji kufanya kazi kwa muda na kuzingatia makubaliano ya mkataba husika kwani Watanzania wanataka maji siyo siasa.

Aidha, mkataba huo umesainiwa kati ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na wazabuni wazawa kampuni nne moja ikiwa na kandarasi mbili ambapo Sh. 8.89 bilioni zitatumika kununua mashine pampu hizo.

Waziri huyo alisema wakati huu si wa kuweka maneno kwenye miradi ya maji bali iwe ni vitendo zaidi ili serikali ijivunie kufanya kazi na makandarasi wazawa.

Vilevile, kiongozi huyo aliagiza kuanzia sasa pampu zifungwe katika maeneo yanayotoa maji hata kabla ya kujengwa kwa matangi ili wananchi waanze kunufaika kuliko kusubiri kwani kumekuwa kunachukua muda mrefu kukamilika.

Mkurugenzi wa RUWASA, Clement Kivegalo, alisema wazabuni waliopewa kazi hiyo watafanya kwa wakati kwa kuwa malipo na stahiki zote katika tenda hiyo zimekuwa tayari kinachoangaliwa ni kazi tu.

Kivegalo alisema namna ilivyo sasa kilio cha maji kinakwenda kuwa historia katika nchi lakini akasisitiza usimamizi wa karibu wa miradi ili iwe na ubora na thamani ya fedha.

Mkurugenzi huo alimhakikishia waziri kuwa RUWASA itafanya kazi usiku na mchana na karibu na wazabuni na makandarasi bila kuchoka hadi waone wanatimiza ndoto ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtoa mwanamke ndoo kichwani.

Akizungumza kwa niaba ya wazabuni James Masage, kutoka kampuni ya Tributa Energy, alisema hakutakuwa na kikwazo ikiwa watapewa malipo ya kazi zao kwa wakati.



## CHADEMA yaipa 5 serikali kwa ujenzi vyumba madarasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Mbeya, kimeipongeza serikali kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa vya kutosha na kusababisha wanafunzi wote waliofaulu mitihani ya darasa la saba mwaka jana kuanza kidato cha kwanza kwa pamoja.

Akizungumza kwenye kikao cha Ushauri cha Ushauri cha Wilaya ya Mbeya (DCC), Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Mbeya Mjini, John Mwambigija, alisema ujenzi wa vyumba vya madarasa hasa kupitia miradi ya UVIKO-19 imesaidia kupunguza mrundikano wa wanafunzi kwenye vyumba vya madarasa.

Vilevile, alisema miradi hiyo imesaidia kuondoa tatizo la wanafunzi kupishana kuanza masomo kama ilivyokuwa inatokea miaka ya nyuma na kusababisha ubora wa elimu nchini kushuka.

Mwambigija aliwapongeza pia viongozi wa Serikali ya Mkoa wa Mbeya na Jiji la Mbeya kwa usimamizi wa miradi hiyo ambayo alisema imekamilika kwa wakati na kuwafanya wanafunzi wote waanze kwa pamoja masomo.

"Tunaipongeza serikali kwa miradi hii na ni mara ya kwanza wanafunzi wote waliofaulu darasa la saba kuanza kwa pamoja masomo, kazi yetu wapinzani huwa ni kuikosoa serikali lakini inapofanya vizuri tunapongeza pia na hili ni miongoni mwa mambo machache tunayoipongeza," alisema Mwambigija.

Aliishauri serikali kuwa na utaratibu wa kuwa na takwimu sahihi za matokeo ya wanafunzi ili iwe rahisi kukabiliana na tatizo la ongezeko la wanafunzi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema katika mkoa mzima wa Mbeya waliletewa fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa 636 katika shule za sekondari na shule za msingi shikizi na kwamba baadhi imekamilika na mingine iko katika hatua za mwisho.

Alisema kwa muda mrefu baadhi ya wanafunzi walikuwa wanachelewa kuanza masomo kwa sababu ya ukosefu wa vyumba vya madarasa, lakini kwa sasa tatizo hilo halipo tena.

Homera alisema mbali na ujenzi wa vyumba vya madarasa pia yametengenezwa madawati ya kutosheleza wanafunzi wote bila kuwapo kwa mrundikano na hakuna wanafunzi watakaokaa chini.

"Tumetoka kwenye zama za wanafunzi kusubiri vyumba vya madarasa, tumeingia kwenye zama za vyumba vya madarasa kusubiri wanafuzi, sasa nawaomba wadau wote wa elimu tushirikiane kuboresha miundombinu mingine," alisema Homera.

Akizungumzia uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza, darasa la awali na kidato cha kwanza, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Ernest Hinju, alisema hali ni nzuri na kuna uwezekano wa kufikia zaidi ya asilimia 100.

Alisema wanafunzi wa kidato cha kwanza walioripoti shuleni wamefikia zaidi ya asilimia 90 huku darasa la kwanza na la awali uandikishaji ukiwa umefikia zaidi ya asilimia 100.

# Viuatilifu visivyokidhi ubora vyakamatwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHEHENA ya viuatilifu visivyokidhi ubora ambavyo vilipigwa marufuku kutumika nchini kikiwamo chenye uwezo wa kuua wanyama wakubwa kama tembo vimekatwa jijini Mbeya vikiuzwa kwa wakulima kwa ajili ya kutumia mashambani.

Hali hiyo inahatarisha usalama wa mazao, wanyama na mazingira.

Shehena hiyo ilikamatwa juzi na maofisa wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Udhibiti wa Viuatilifu (TPHPA) waliposhirikiana na makachero wa Jeshi la Polisi kufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka ya viuatilifu.

Mkaguzi wa Viuatilifu wa TPHPA, Mkalasa Kubila, alisema moja kati ya viuatilifu walivyovikamata ni karate, dawa ya kuulia panya aina ya Latox na Carbon fulate ambacho kimepigwa marufuku kutumika nchini.

Alisema aina zingine za viuatilifu hivyo zilikamatwa kutokana na kwamba havijathibitishwa ubora wake na taasisi hiyo lakini kiuatilifu aina ya Carbon kimepigwa marufuku kutumika nchini.

"Viuatilifu hivi vimeingizwa nchini kupitia njia zisizokuwa rasmi, na kwa mujibu wa sheria kiuatilifu cha aina yoyote kinapoingizwa nchini ni lazima tukithibitishe ubora wake na msambazaji lazima apate kibali kutoka kwetu lakini hivi viuatilifu wanaviuza bila kuwa na vibali," alisema Kubila.

Alisema viuatilifu ambavyo havijaruhusiwa kutumika nchini ni hatari kwenye mazingira na kwa viumbe vingine na hivyo akawataka wafanyabiashara kuepuka kuviuza kwa wakulima.

Baadhi ya wauzaji wa viuatilifu hivyo walisema waliviingiza kutoka nje ya nchi, lakini walikuwa hawajui kama haviruhusiwi kuuzwa nchini na kwamba ndio maana waliamua kuviuza kwenye maduka yao licha ya kutokuwa na nembo ya TPHPA.

Moja wa wauzaji hao, Furaha Kyamba, alisema viuatilifu hivyo waliletewa kutoka nchini Zimbabwe na hawakujua kwamba haviruhusiwi kisheria kuuzwa nchini.

Alisema wafanyabiashara waliomletea walimshawishi kuwa ni viuatilifu vizuri na vina soko, hivyo yeye akaamua kuvichukua akiamini kuwa ni biashara halali mpaka alipokutwa na maofisa wa TPHPA ndipo alipojua kwamba haviruhusiwi kuuzwa.

"Nawashauri wafanyabiashara wenzangu waache kuuza viuatilifu kama hivi ambavyo havikubaliki nchini, ukikamatwa ni hatari sana maana unaweza ukafilisiwa mtaji wote na pengine ukafungwa, mimi sitarudia tena kuviuza," alisema Furaha.

Ofisa Mfawidhi wa TPHPA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Mausa, aliwataka wakulima kununua viuatilifu ambavyo vimesajiliwa na mamlaka hiyo kwa kuangalia nembo kwa maelezo kuwa ndivyo vinavyoruhusiwa kisheria.

Alisema taasisi hiyo ndiyo inayothibitisha ubora wa viuatilifu kwa kuangalia ubora wake na madhara yake kwenye mimea, mazingira na wanyama hivyo wakulima wakikuta havijathibitishwa wanatakiwa kuviepuka na ikiwezekana watowe taarifa.

Vilevile aliwataka wafanyabiashara kuacha kuuza viuatilifu ambavyo haviruhusiwi kuuzwa nchini ili kuepuka mkono wa sheria ikiwamo kupelekwa mahakamani na kutozwa faini.

Shehena ya viuatilifu hivyo ambavyo vilikamatwa ilichukuliwa na maofisa wa taasisi hiyo kwa ajili ya hatua zingine za kisheria dhidi ya wafanyabiashara waliokamatwa.



Meya wa Jiji la Mbeya, Dormohamed Issa (katikati), akisoma dua wakati wa kufungua kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji hilo cha kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Kushoto ni Mkurugenzi wa Jiji hilo, Amede Ng'wanidako na Naibu Meya wa Jiji hilo, Agness Mangasila (kulia). **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Jiji kuongeza makusanyo ya mapato

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, inatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 88.3 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na matumizi mengine katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, huku makusanyo ya ndani yakitarajiwa kuongezeka.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, Amede Ng'wanidako, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye Mkutano Maalumu wa Baraza la Madiwani la kupita na kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Bajeti ya Halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha ujao.

Ng'wanidako alisema katika bajeti hiyo makusanyo ya ndani ya halmashauri hiyo yataongezeka kutoka Sh. bilioni 16.7 mpaka Sh. bilioni 18.3 na kwamba makusanyo hayo yanatarajiwa kuongezeka kutokana na ongezeko la vyanzo vya mapato.

Alisema kwenye bajeti hiyo wameweka vipaumbele nane ambavyo fedha hizo zitaelekezwa ikiwamo ujenzi wa shule mpya na ukarabati wa zilizochakaa.

Vilevile, alisema katika bajeti hiyo wanakusudia kununua gari moja maalumu kwa ajili ya kuzolea taka, kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa sheria za nchi.

Pia alisema wanakusudia kujenga kituo kimoja cha afya ambacho kitajengwa katika Kata ya Isyesye na ujenzi wa shule moja maalumu ya sekondari kwa ajili ya wanafunzi wa kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne.

"Vipaumbele hivi na bajeti yetu nzima ni kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma bora kwa jamii yetu, ili tufanikishe haya ni lazima tuwe na ushirikiano wa kutosha baina ya madiwani na watumishi wote wa halmashauri yetu," alisema Ng'wanidako.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini, Afrey Nsomba, aliwapongeza madiwani wa jiji hilo pamoja na watendaji wa jiji hilo kwa ushirikiano walioonyesha hasa kwenye usimamizi wa matumizi.

Alisema chama hicho kinafurahishwa na namna madiwani hao wanavyofanya kazi kwa ushirikiano na kwamba hali hiyo ndiyo inawafanya madiwani wa halmashauri zingine kwenda kujifunza namna ya utekelezaji wa miradi.

Aliwataka madiwani hao kwenda kuwaelewesha wananchi wa maeneo yao kuhusu bajeti hiyo ili wawe na uelewa kuhusu namna ambavyo serikali inapanga kuwahudumia.

"Sisi chama tunaendelea kufuatilia mabaraza yote na kwa Halmashauri yetu ya Jiji la Mbeya tunafurahishwa sana na namna mnavyofanya kazi, nawaomba kwa niaba ya chama mwendelee kushirikiana katika kuwahudumia wananchi wetu," alisema Nsomba.

Kwa upande wake Meya wa Jiji hilo, Sheikh Dormhamed Issa,



# Miradi uwekezaji kimkakati kukaguliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itahakikisha itaunda timu maalum ya wataalamu kukagua miradi yote ya uwekezaji wa kimkakati ambayo imepewa misamaha ya kodi ili kuhakikisha misamaha hiyo inatumiwa ipasavyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, aliyasema hayo wakati wakitembelea mradi wa Hoteli ya Emerald Zanzibar Resort and Spa Zanzibar huko Muyuni Beach Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema timu hiyo ikiweza kufanya kazi itatoa uelewa mpana juu ya hali halisi ya mapato yanayokusanywa na mapato yanayopotea katika sekta hiyo ya utalii hususan katika kipindi cha ujenzi wa hoteli hizo.

"Mtu anaweza kusema anajenga hoteli ya vyumba 50 na katika michoro akaonyesha lakini siku unaenda unakuta amejenga vyumba 10 na tumesamehe kodi katika nondo na saruji," alisema.

Waziri Jamal aliwataka makamishna wanaohusika na masuala ya ukusanyaji wa kodi kuhakikisha wanaunda timu maalum ya ufatiliaji wa kampuni ndogo zilizokuwapo kwenye miradi mikubwa ya kimaendeleo kuona zimesajiliwa na kutafuta utaratibu wa kuzisajili ili kodi ya serikali inapatikana kama ilivyokusudiwa.

Waziri Jamal alisema kwamba hivi sasa kuna tatizo kubwa katika kipindi cha ujenzi ya miradi mikubwa na hakuna fedha yoyote ambayo inaingia serikalini inayotakiwa kulipwa. Alisema baada ya timu hiyo kupeleka ripoti itakabidhiwa kwa wataalamu ili kuhakikisha kodi yote inayostahiki inalipwa na kama kutakuwa na mtu ambaye amekiuka matumizi yake, serikali itafuata sheria katika jambo hilo.

Akizungumzia mradi wa Hoteli ya Palolo, alisema umepewa uwekezaji wa kimkakati katika kodi ili kuchochea uwekezaji wa miradi mikubwa ya aina hiyo na Zanzibar ni sehemu ya nchi yenye fursa kubwa ya utalii.

Naye Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Salum Yussuf Ali, aliahidi kulifanyia kazi suala hilo na serikali imekuwa ikitegemea mapato hayo katika kuhudumia wananchi kupata huduma bora.

Kwa upande wake Meneja Mradi wa Ujenzi wa Hoteli ya Palolo Altedo Otri, alisema wao ni wadau wakubwa katika ulipaji wa kodi kwa serikali.



Baadhi ya waandishi wa habari Zanzibar wakiwa katika mafunzo kuhusu kuandika habari za utatuzi wa migogoro, mafunzo ambayo yameandaliwa na kituo cha huduma na sheria Zanzibar kupitia mradi wa jenga amani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jafo: Sijaridhishwa kutokamilika visima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Mungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema hajaridhishwa na kitendo cha kucheleweshwa kukamilika kwa visima sita katika shehia tatu za Matemwe Mbuyu Tende, Kijini na Jugaleni Wilaya ya Kaskazini Unguja.

Alisema kuchelewa kuanza kwa hatua za awali za ujenzi wa visima hivyo kunarejesha nyuma maendeleo ya wananchi katika shehia husika kwa vile lengo ni kuwapatia wananchi majisafi na salama katika shehia hizo na hata kufanya shughuli za umwagiliaji maji.

Alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua mradi wa uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mfumo wa ikolojia vijijini huko Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema mradi huo una umuhimu katika kukamilika kwa wakati uliopangwa ili kuleta faida kwa wananchi.

Alisema mradi kama huo kwa upande wa Tanzania Bara kwa kiasi kikubwa umeshatoa sura kwa kuchimbwa kwa visima na kuweka matangi ili ibaki kazi ya kusambaza kwa wananchi na ndiyo lengo la mradi huo.

Waziri Jafo alisema kitendo cha kuchelewa kwa visima hivyo hakivumiliki na kazi kubwa iliyoko kwa sasa lazima mkandarasi atakayepewa kupangiwa muda wa kumalizika kwa wakati kwa sababu mradi huo unatarajiwa kukamilika muda wake Juni 30, mwaka huu.

Alisema kuwa wataalamu wa kuwatafuta makandarasi wa visima hivyo lazima wawe makini kwa kuwasimamia ambao watapewa kazi hiyo na iwapo hawajakamilisha kwa watakati wasionewe haya kusitishiwa mkataba.

Kwa upande wa mazingira juu ya mradi huo, alisema wananchi wanatakiwa kufahamu kuwa mazingira yanatakiwa kulindwa kwa gharama yoyote ili kuondosha ukame na kuondoa mabadiliko ya nchi kuwa jangwa.

Alisema katika mradi huo wa kimazingira wananchi wanatakiwa kutumia fursa za kutumia miti kuweka nafasi ya kujipatia uchumi ikiwamo wa kutengezea sabuni, dawa za kuasishia vyoo na kutengeza vitu vya asili vya manukato.

Jafo alisema uamuzi wa wanakikundi cha Matemwe na ujasiriamali kutumia miti kutengeneza bidhaa mbalimbali ni moja ya kujipa hali ngumu ya umaskini.

Aidha, waziri huyo alitembelea Kijiji cha Matemwe na kuona maji ya bahari yakipanda katika maeneo ya juu ya makazi ya wananchi na kusema kuwa ofisi yake itakaa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar kujadili juu ya uharibifu huo.

Alisema hali ya mazingira hivi sasa imekuwa inahatarisha maisha ya viumbe katika baadhi ya maeneo kuwa ya jangwa.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema mradi huo umetoa nafasi kwa baadhi ya wananchi kujiajiri na kujipatia kipato ii kunufaika na miti asili.

Alisema mradi huo wa miaka mitano. unaonekana kuwa una faida kubwa kwa wananchi katika harakati zao za kila siku kwa sababu moja ya kutunza mazingira.

Alieleza kuwa hivi sasa wananchi wanatakiwa kutumia majiko sanifu ili kutunza mazingira na kuepukana na mabadiliko ya tabianchi.

Wakazi wa shehia hizo walisema kupatikana kwa mradi huo kumetengeneza nafasi za ajira kwa vijana na wanawake na kujikimu kimaisha.

## China yaeleza lengo msaada kwa jumuiya

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

BALOZI wa China nchini, Zhang Zhisheng, amesema msaada wa vyerehani uliotolewa na Ubalozi huo kwa Jumuiya ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, unalenga kuwawezesha wanawake wa Zanzibar ili kuondokana na umaskini.

Balozi Zhang alisema hayo alipokabidhi vyerehani vinane kwa uongozi wa Jumuiya ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, katika hafla iliofanyika ubalozi huo Mazizini Zanzibar.

Alisema msaada wa huo ni mwanzo wa misaada mbalimbali inayolengwa kutolewa na ubalozi huo kwa jumuiya hiyo ili kuwawezesha wanawake wa Zanzibar kuinua maisha yao.

Naye Mtendaji Mkuu wa Jumuiya hiyo, Mwanaidi Mohamed Ali, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo ambaye ni mke wa Rais wa Zanzibar, Mariamu Mwinyi, aliushukuru Ubalozi wa China kwa msaada huo, na kusema hatua hiyo inaonyesha dhamira ya katika kushirikiana na jumuiya hiyo, ili kuwawezesha wanawake Zanzibar.

Alisema Jumuiya ya Zanzibar Maisha Bora Foundation inathamini msaada huo na itaendelea kushirikiana na ubalozi huo, huku akiahidi kutumika vyema kwa malengo yaliokusudia.

Msaada unatokana na mkutano wa wadau uliofanyika Januari 26, mwaka huu mjini Zanzibar, uliolenga kuwahamasisha wadau mbalimbali kushirikiana na jumuiya hiyo ili kufanikisha malengo yaliokusudiwa.

Jumuiya ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, ambapo malengo yake makuu ni kuinua maisha ya wanakake wa Zanzibar kuondokana na umaskini, inatarajiwa kuzinduliwa rasmi mwezi ujao.

# Mwanza yataja sababu kufanya vizuri kwenye chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Ruta Thomas, amesema, kilichoufanya mkoa wake kuwa miongoni mwa mitano inayofanya vizuri katika chanjo ya UVIKO-19, ni ushirikishaji wa wadau wote kuanzia ngazi ya jamii.

Akizungumza na Nipashe jana, Mganga huyo alisema, mkoa huo unashirikiana kwa karibu na wahudumu wa afya kuanzia ngazi ya jamii na viongozi wa serikali za mitaa, kwa ajili ya uhamasishaji wa chanjo hiyo.

"Pamoja na hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza amekuwa akipokea taarifa za kila siku kutoka kila halmashauri kwa kuwa ndizo zenye jukumu la kusimamia jambo hilo, lakini kuna kamati ya amani ya mkoa," alisema Dk. Thomas.

Alisema, kamati hiyo ambayo iko chini ya viongozi kutoka madhehebu mbalimbali, jukumu lao ni kuhimiza amani na upendo, na kwamba imekuwa ikisaidia kuhamasisha watu kuchanja.

"Mkoa wetu una vituo 346 vya chanjo ambavyo viko kwenye halmashauri nane ambazo ni Kwimba, Sengerema, Buchosa, Ukerewe, Ilemela, Misungwe, Magu na Manispaa ya Jiji la Mwanza," alisema.

Dk. Thomas alifafanua ofisi yake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaendelea kutoa chanjo kwa wakazi wa mkoa huo katika vituo hivyo 346, ili kuwakinga dhidi ya ugonjwa huo.

"Tunaendelea kusisitiza watu kuchukua tahadhari zote ambazo zinaelekezwa, ikiwamo kuvaa barakoa, kunawa maji tiririka, kutumia vitakasa mikono na pia kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima," alisema.

Mwanza ni miongoni mwa mikoa mitano iliyowahi kutajwa na aliyekuwa Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, kuwa inaongoza kwa chanjo ya UVIKO-19, huku mingine ikiwa ni Ruvuma, Mara, Kagera na Dodoma.

Mbali na kutaja mikoa hiyo, akafafanua kuwa tangu chanjo ilipozinduliwa mwishoni mwa Julai mwaka jana, kufikia Desemba 18 mwaka huo, watu 1.27 walikuwa wameshapata chanjo kamili ya kujikinga na UVIKO-19.

Aidha, katika taarifa yake hiyo, waziri huyo alitaja mikoa inayodaiwa kufanya vibaya katika utoaji wa chanjo kuwa ni Manyara, Songwe, Njombe, Singida na Iringa na kuitaka iongeze kasi.



Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (katikati), akizungumza jana na watumishi wa Kituo cha Afya Makorola jijini Tanga ikiwa ni ziara ya kukagua vituo vya afya jijini humo. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

## Radi yateketeza nyumba, yajeruhi wanne Mtwara

**Na Hamisi Nasri,** NEWALA

MOTO uliosababishwa na radi umeteketeza nyumba na mali zote na kujeruhi watu wanne katika Kijiji cha Tengulengu, Kata ya Mkwedu, Halmashauri ya Wilaya ya Newala mkoani Mtwara.

Akizungumza na gazeti hili kijijini hapo, Mwenyekiti wa serikali ya kijiji kwa masharti ya kutoandikwa majina yake gazetini, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa limetokea juzi majira ya saa saba mchana baada ya mvua iliyoambatana na radi za mara kwa mara.

Alimtaja mkazi aliyeunguliwa na nyumba kuwa ni Hassan Namtema, kitongoji cha Azimio katika kijiji hicho.

Alisema ndani ya nyumba hiyo kulikuwa na watu wengine saba na kati yao wanne walijeruhiwa na radi hiyo.

Aliwataja waliojeruhiwa kuwa ni Sina Seifu, Amina Ismail, Juma Gayo na Hasasan Namtema ambao walikimbizwa katika zahanati ya kijiji hicho.

Akizungumza na baadhi ya viongozi waliofika katika eneo la tukio akiwamo Diwani wa Kata ya Mkwedu, Akayoha Hamisi, aliyeunguliwa nyumba alisema, wakati mvua ikinyesha alikuwa ndani ya nyumba ndipo radi kubwa ilipopiga na kuwaka moto ulioshika katika nyumba yake.

"Nilikuwa ndani ya nyumba yangu nimekaa ndipo niliposikia mshindo mkubwa umepiga katika nyumba yangu na ghafla niliona moto ukiwaka katika paa la nyumba nikiwa na wenzangu ndani tulikimbilia nje haraka," alisema Namtema.

Naye diwani wa kata hiyo, Akayoha Hamisi, alisema ameshuhudia nyumba hiyo ilivyoteketea vikiwamo vyakula na mali zote.

# AfDB yamtaka mkandarasi kukamilisha mradi umeme

**Na Peter Haule,** ARUSHA

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imemtaka mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa umeme wa Singida-Arusha hadi Isinya nchini Kenya unaogharimu dola za Marekani milioni 258 zilizotolewa kwa mkopo na benki hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) na Serikali ya Tanzania, kuharakisha utekelezaji wa mradi huo ili ifikapo Desemba mwaka huu uweze kukamilika.

Rai hiyo imetolewa jijini Arusha na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo anayesimamia nchi tisa za Afrika ikiwamo Tanzania, Kenya, Ethiopia, Rwanda, Seychelles, Sudan Kusini, Eritrea Uganda na Somalia katika benki hiyo, Amos Cheptoo, alipotembelea na kukagua mradi wa kituo cha umeme cha Lemugur, mkoani Arusha, ambacho ni sehemu ya mradi mkubwa wa umeme wa Singida- Arusha hadi Isanya Kenya.

Cheptoo ambaye yuko nchini kwa ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi iliyopata fedha za mkopo nafuu kutoka benki hiyo upande wa Zanzibar na Tanzania Bara, alisema ni vema mradi huo ukakamilika kwa wakati ili uweze kutoa huduma zitakazochochea maendeleo kwa nchi za Afrika hususani Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

"Sekta ya umeme ni muhimu katika kuchochea kwa haraka maendeleo ya biashara katika nchi za Afrika, miundombinu ya umeme nchini Tanzania ikiunganishwa na ile ya Kenya ambayo tayari imeunganika na Ethiopia na upande mwingine wa Tanzania imeunganishwa na Zambia, itasaidia biashara ya nishati hiyo kufanyika kwa haraka katika upande wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika," alisema Cheptoo.

Alisema nishati ya umeme imepewa kipaumbele kikubwa na AfDB kutokana na umuhimu wake, hivyo asilimia 16 ya uwekezaji unaofanywa na benki hiyo nchini Tanzania ni ya nishati hiyo.

Cheptoo alisema zipo sekta nyingine ambazo zinamanufaa makubwa kwa ukuaji wa uchumi katika Bara la Afrika kama sekta ya ujenzi hususani katika uwekezaji wa miundombinu ya reli, lakini uwekezaji wake una gharama kubwa ikilinganishwa na miundombinu ya nishati ya umeme.

Mratibu wa Mradi wa Umeme kati ya Tanzania na Kenya (KTPIP), Peter Kigadye, alisema kuwa mradi huo wa umeme unaounganisha Tanzania na Kenya, ni sehemu ya mradi mkubwa wa kuunganisha umeme katika nchi za Afrika Mashariki kutokea Ethiopia na Kenya ambao unaunganishwa na Kituo cha Lemugur-Arusha na Isinya upande wa Kenya.

Alisema mradi huo ni sehemu ya mradi wa pili mkubwa wa Msongo wa Umeme wa Kilovoti 400 wenye kilomita 670 kutoka Iringa hadi Shinyanga ambao unaunganishwa na Singida -Arusha kuelekea Isanya nchini Kenya.

Alisema mradi wa umeme wa Kenya na Tanzania ni wa msongo wa Kilovoti 400 kwa kilomita 510 ambapo kilometa 414 ni upande wa Tanzania na kilometa 96 kutoka mpaka wa Tanzania na Kenya (Namanga) hadi Kituo cha Isinya nchini Kenya.

## HABARI KITAIFA

# Waliounguliwa soko Dar sasa kupigwa msasa

**Na Christina Mwakangale**

WATAALAMU wa Ustawi wa Jamii na Saikolojia kutoka Kituo cha Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia kilicho chini ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii, wametoa elimu na ushauri kwa wafanyabiashara wa soko la Mchikichini, waliounguliwa bidhaa zao na maeneo ya biashara.

Huduma hiyo ilitolewa bure kwa wafanyabiashara wa soko hilo maarufu Karume, jijini Dar es Salaam, wakiwalenga kundi maalum, ambalo ni waathiriwa wa moto, tukio lililotokea Januari 16, mwaka huu. Mratibu wa kituo hicho, Rufina Khumbe akizungumza mwishoni mwa wiki, alisema Taasisi ya Ustawi wa Jamii, iliona ni vyema kutoa huduma hiyo kwa waathirika hao, ambao wanauhitaji mkubwa kwa wakati huu.

"Taasisi imekuwa ikitoa huduma kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ili kuhakikisha tunastawisha jamii yetu, kwa kutatua changamoto mbalimbali pia kama taasisi mama chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

"Tumeguswa na ni jukumu la kituo chetu cha ushauri kuja kutoa huduma ya elimu hii na ushauri, ili wafanyabiashara hawa hasa wenye uhitaji waweze kulipokea hilo na kulikubali kama changamoto," alisema Rufina.

Rufina alisema, kutokana na janga hilo la moto wengi wao wamekata tamaa ya maisha, kwa sababu mali zilizokuwa zinawaingizia kipato na mitaji, vimeteketea kwa moto huku wengine wakichukua mikopo ili kukuza na kuanzisha biashara.

"Mali zimeteketea na hawajui wanalipaje hiyo mikopo. Ndio maana taasisi ikaona ni vyema kuongea na wafanyabiashara hawa, ili kuwapa tumaini tena la maisha yao," alisema Rufina.

Msaikolojia kutoka kituo hicho, Zainabu Rashidi alisema kwamba, ipo dhana ya baadhi ya waathiriwa kudhani elimu ya ushauri na kisaikolojia inakwenda pamoja na kutopata msaada wa fedha kwa ajili ya mitaji yao ya biashara.

"Tunatoa elimu juu ya kujikinga na majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na moto, mafuriko na pia tunatoa elimu ya namna ya kuyakubali na kuishi na majanga na matatizo baada ya kutokea.

"Jamii yetu haina uelewa juu ya umuhimu wa huduma ya ushauri na msaada wa kisaikolojia kama tiba ya namna ya kupata suluhu ya matatizo yao kwa kuzungumza na wataalam. Jamii haiamini katika ushauri pekee hivyo tuko hapa ili kuondoa hiyo dhana," alisema Zainabu.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wenye Ulemavu Soko la Mchikichini, Juma Hamisi, alisema anashukuru taasisi ya ustawi wa jamii kwa elimu, ushauri, na msaada wa kisaikolojia.

# TBS yateketeza vipodozi vya mil. 70/-

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) ofisi za Kanda za Kaskazini limeteketeza vipodozi vya aina mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 70 vilivyopigwa marufuku kwa matumizi ya binadamu nchini.

Vipodozi hivyo vilivyoteketezwa mwishoni mwa wiki jijini hapo, vilikamatwa na kuondolewa sokoni kwa nyakati tofauti katika mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari, vipodozi hivyo vimepigwa marufuku kutumika kwa matumizi ya binadamu kutokana na kuwa na viambata sumu ambavyo huweza kudhuru afya ya mtumiaji.

Baadhi ya bidhaa zilizokamatwa zenye viambata sumu ziko kwenye makundi tofauti kutoka nje ya nchi.

Taarifa hiyo ilieleza kwamba bidhaa hizo zinakadiriwa kuwa na thamani ya Sh. milioni 70 kwa bei ya rejareja sokoni. Utafiti wa bei ya bidhaa hizo ulifanywa kwa kuuliza wauzaji zinapokamatwa.

Sheria ya Viwango No: 2 ya mwaka 2009 ikisomwa pamoja na kanuni ya usajili wa majengo yanayojihusisha na uuzaji wa vyakula na vipodozi pamoja na usajili wa bidhaa Kifungu cha 14 (1) kinakataza uuzaji, usambazaji na uhifadhi wa vipodozi vilivyopigwa marufuku.

Taarifa hiyo ilitaja athari ya vipodozi vyenye viambata sumu kuwa husababisha kansa ya ngozi pamoja na madhara mengine kama ya ngozi kuwa nyembamba na laini sana kiasi cha kushindwa kushoneka mtumiaji anapopata ajali.

Madhara mengine ni sumu kupenya kwenye ngozi na kuingia kwenye mishipa hasa kichwani, kusababisha madhara ya figo na kwa wajawazito sumu inaweza kuathiri mtoto aliye tumboni.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza madhara mengine huweza kujitokeza baada ya muda mrefu.

Shirika hilo limewataka wananchi kuacha kutumia vipodozi vilivyopigwa marufuku kwa kuwa huleta madhara kwa nguvu kazi ya taifa kupindi mtu anapoathirika na hulazimika kutumia gharama kubwa kujitibu na muda mwingi hupotea kwa kushindwa kujenga taifa.

"Kila Mtanzania awe mkaguzi wa bidhaa hizi tunasisitiza ukaguzi uanzie ndani mwetu sisi wote," ilieleza taarifa hiyo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akipanda mti aina ya mkoko katika hafla ya uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti aina ya mikoko katika delta ya Mto Rufiji. Uzinduzi huo umefanyika mwishoni mwa wiki katika Kijiji cha Mbuchi, Tarafa ya Mbwela, Wilaya ya Kibiti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Nchi haitakuwa gizani mgawo ukianza'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANANCHI wametakiwa kuondoa hofu iliyojengeka kuhusu maboresho yanayofanywa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwamba hayatasababisha nchi kuingia gizani.

Maboresho hayo yanafanyika ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa huduma ya nishati ya umeme, hivyo Watanzania wasiwe na shaka ya mgawo wa umeme nchi haitaingia gizani.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amesema maboresho hayo ya siku kumi hayawezi kuingiza nchi kwenye giza, na kwamba ni ya kawaida kufanyika.

Msigwa aliyaeleza hayo jana mjini Kibaha alipokuwa akizungumza na waandishi pamoja na maofisa habari wa mkoa wa Pwani kuhusiana na taarifa ya miradi ya maendeleo ya mkoa huo.

"Watu waache kuwajaza hofu Watanzania, linalofanyika ni maboresho ya kawaida kwenye mitambo na hakuna athari itakayotokea," alisema.

Akizungumzia kuhusiana na miradi ya maendeleo katika mkoa wa Pwani, alisema zaidi ya Sh. bilioni 298.3 zimetengwa kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 na kwamba kwa kupindi cha awamu ya sita tayari Sh. bilioni 241 zimetolewa.

Alisema serikali imeendelea kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Umma ambapo kuanzia mwezi Machi 2021 hadi mwezi Januari 2022, imelipa madai ya watumishi 65,391 ya Sh. bilioni 90.7.

Akizungumzia upande wa ardhi, Msigwa alisema serikali imejipanga kuondoa kero inayowakumba Watanzania ya kupata hatimiliki.

Alisema serikali iliamua kuharakisha utoaji wa hati kwa kutoa mkopo wa Sh. bilioni 50 kwa Wizara ya Ardhi na kwamba mpango huo umefanikisha kupima viwanja 210,904 katika halmashauri 60 nchini.

Kwa upande wa maeneo ya uwekezaji alisema hekta zaidi ya 53 zimetengwa na jitihada za serikali ni kuhakikisha wawekezaji katika sekta ya viwanda wanaongezeka kukuza uchumi wa Taifa na ajira kwa vijana.

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka ya sasa Tarehe 31/12/2021 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/09/2021 |
|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS |
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 84 | 89 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 10,671 | 11,770 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushungulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima ya Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | | - | - |
| | Mikopo Halisi Iliyopo | 19,426 | 18,166 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,517 | 2,763 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika ,Mitambo na Vifaa | 1,510 | 1,552 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **34,208** | **34,340** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 1,483 | 1,618 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 3,923 | 3,687 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 797 | 798 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 669 | 995 |
| 27 | Zitakazolipwa Baadae | 1,526 | 1,737 |
| 28 | Dhima Nyingine | - | - |
| **29** | **Madeni** | **8,398** | **8,835** |
| | **JUMLA YA DHIMA** | | |
| **30** | **MALI/(DHIMA)HALISI (16 kutoka 29)** | **25,811** | **25,505** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,200 | 21,200 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 12 | 12 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,199 | 1,259 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,288 | 916 |
| 35 | Akauti Nyingine za Mtaji | 2,112 | 2,118 |
| 36 | **Stahiki ya Wenyehisa Chache** | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISANI** | **25,811** | **25,505** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | **499** | **559** |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | **390** | **448** |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | **75%** | **74%** |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | **2.5%** | **3.1%** |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **364%** | **342%** |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Hali na Mali | **58%** | **53%** |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | **58%** | **69%** |
| (vi) | Ongezeko la Amana | **1.9%** | **-2.5%** |
| (vii) | Ongezeko la Mali | **-0.4%** | **0.7%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 31/12/2021 | Robo ya Mwaka Linganishi 31/12/2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31/12/2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31/12/2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 | Mapato ya Riba | 2,438 | 2,126 | 9,853 | 9,194 |
| 2 | Gharama za Riba | 2 | 11 | 14 | 29 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2 )** | **2,436** | **2,116** | **9,839** | **9,165** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (469) | **0** | (712) | **(857)** |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,143** | **598** | **2,430** | **2,223** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 20 | (1) | 3 | (1) |
| | 6.2 Ada za Kamisheni | 857 | 336 | 1,734 | 1,317 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 266 | 263 | 693 | 907 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba :** | **2,686** | **2,595** | **10,059** | **10,711** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 1,214 | 1,165 | 4,828 | 5,245 |
| | 7.2 Gharama Nyingine | 1,472 | 1,431 | 5,231 | 5,465 |
| | 7,3 Ada na Kamisheni | | | | |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **425** | **118** | **1,498** | **(179)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 53 | - | 210 | - |
| **10** | **Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **372** | **118** | **1,288** | **(179)** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | **275** | **256** | **275** | **256** |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 17,551 | 5,573 | 60,763 | (8,798) |
| 13 | Kipato kwa Hisa | 17,551 | 5,573 | 60,763 | (8,798) |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15 | Vituo Vya Biashara | 36 | 54 | 36 | 54 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | 1.1% | 0.4% | 3.8% | -0.5% |
| (ii) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.5% | 0.5% | 5.0% | -0.8% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 75% | 96% | 82% | 94% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani Wa Mali Zinazozalisha | **22%** | **24%** | **91%** | **62%** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Mwaka (2021)** | **21,200** | **1,447** | **0** | **2,206** | **24,853** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **1,288** | - | - | **1,288** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | **(248)** | - | **(82)** | **(330)** |
| **Salio la mwisho wa Robo ya mwaka wa sasa** | **21,200** | **2,487** | **0** | **2,124** | **25,811** |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka Uliopita ( 2020)** | **21,200** | **1,657** | **190** | **2,566** | **25,613** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **(179)** | - | - | **(179)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | **190** | **(190)** | - | - |
| Mengineyo | - | **(220)** | - | **(360)** | **(581)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **21,200** | **1,447** | **0** | **2,205** | **24,853** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 31/12/2021 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/09/2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31/12/2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31/12/2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| **I:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | | | |
| | Mapato/(Hasara)Hakisi | **372** | **249** | **1,288** | **(179)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | | | |
| | Hasara Katika Mali | 159 | 123 | 504 | 352 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,260) | (29) | (3,646) | 5,858 |
| | Faida/Hasira Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 101 | (139) | 825 | (1,530) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 245 | (110) | 1,187 | (760) |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo | (538) | 129 | (469) | 1,878 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | - | - | - | - |
| | **kwa shughuli za uendeshaji** | **(921)** | **224** | **(310)** | **4,023** |
| **II:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTIKANA NA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI** | | | | |
| | Gawio Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (117) | (111) | (308) | (362) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | | | | |
| | **kwa Shughuli za uekezaji** | **(117)** | **(111)** | **(308)** | **(362)** |
| | | - | - | - | - |
| **III:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULIZA KIFEDHA** | - | - | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo | (66) | - | (330) | (581) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| | **kwa Shughuli za Kifedha** | **(66)** | **-** | **(330)** | **(581)** |
| **IV:** | **FEDHA TASLIMU NA MALI ZAINAZOFANANA NA FEDHA TASLIMU** | | | | |
| | Onzezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofana na Fedha Tastimu | (1,104) | 113 | (949) | 3,081 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 11,859 | 11,746 | 11,703 | 8,622 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu /** | | | | |
| | **Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **10,754** | **11,859** | **10,754** | **11,703** |

Katika kuaandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mwijage B Bishota (Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu) | | 20 Januari 2021 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha ) | | 20 Januari 2021 |
| Modest Kissima (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | | 20 Januari 2021 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifaza zahapo juu,Tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Athanasia Soka ( Mwenyekiti wa Bodi)** | | 20 Januari 2021 |
| **Loyce Isanzu (Mwendeshaji)** | | 20 Januari 2021 |

# ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA

**ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA**

| Huduma za Kibenki | | | Gharama-Pamoja na VAT (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuangalia Salio-Dirishani | | 554 |
| 2 | Kuhamisha fedha | Ndani ya VFT hadi TZS1,000,000 | 944 |
| | | Ndani ya VFT zaidi ya TZS1,000,000 | 1,180 |
| | | Kwenda Benki nyingine hadi TZS10,000,000 | 3,554 |
| | | Kwenda Benki Nyingine zaidi ya TZS10,000,000 | 11,800 |
| 3 | Kutoa disrishani hadi TZS 5,000,000 | | 1,770 |
| 4 | Kutoa ATM | | 1,500 |
| 5 | Kubadili Kadi ya ATM | | 5,000 |
| 6 | Taarifa Fupi ATM | | 472 |
| 7 | Gharama za mwezi (Monthly Acc maintanance fees) | Akiba Account | 885 |
| | | Business account | 1,770 |
| 8 | Kufunga Akaunti | Akaunti ya Akiba, Watoto & Dunduliza | 2,360 |
| | | Akaunti ya vikundi na Biashara | 5,900 |
| 9 | Taarifa ya Akaunti | Taarifa Fupi ATM | 720 |
| | | Miezi 0-3 | 1,180 |
| | | Miezi 3-12 | 3,540 |
| | | Miezi 12-24 | 11,800 |
| | | Miezi 24-48 | 29,500 |
| | | Miaka 3-6 | 41,300 |
| | | Zaidi ya miaka 6 | 55,400 |

| Huduma Za Simu (Mobile banking) | | Pamoja na VAT (TZS) |
|---|---|---|
| 9 | Kujua Salio-Simu | 118 |
| 10 | Kutoa-Simu | Bure |
| 11 | Kuhamisha Fedha-Simu | 118 |
| 12 | Taarifa Fupi-Simu | 354 |
| 13 | Kubadili Number ya Siri | 236 |

**Akaunti**

| s/n | Huduma | Kiwango cha chini | Riba Kwa mwaka * |
|---|---|---|---|
| 1 | Akiba Accounts | 5,000 | 4% |
| 2 | Joint Accounts | 5,000 | 4% |
| 3 | Group Accounts | 20,000 | 4% |
| 4 | Watoto Accounts | 10,000 | 4% |
| 5 | Bussiness Accounts | 100,000 | 4% |
| 6 | Fixed Deposit Accounts | N/A | Kulingana na muda na Kiasi |
| 7 | Dunduliza Accounts | 10,000 | Kulingana na muda na Kiasi |

** Riba kwa akaunti za aina zote itajilimbikiza kwa kila la siku kwa kiasi cha akiba cha TZS100,000 na kuendelea.*

**Mikopo ya Vikundi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Biashara Loan | 5% | 60% | 3% |
| 2 | Group Savings Group Loan | 5% | 60% | 2.5% |
| 3 | Group Jiendeleze | 4% | 48% | 3.5% |

**Mikopo Binafsi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Mkopo Binafsi- hadi TZS10M | 4% | 48% | 2.5% |
| 5 | Mkopo Binafsi inayozidi TZS10M Hadi TZS 20M | 3.50% | 42% | 2.5% |
| 6 | Mikopo Binafsi inayozidi TZS20M | 2.50% | 30% | 2.5% |
| 7 | Elimisha | 4% | 48% | 3.5% |

**Mikopo ya Kilimo**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Jikomboe | 4% | 48% | 5% |
| 10 | Jitume | 5% | 60% | 5% |
| 11 | Mkombozi | 5% | 60% | 5% |
| 12 | Patnerships | Negotiable | Negotiable | Negotiable |

**13. Gharama za kutoa kwa wakala Kuanzia tarehe 1 Machi 2022**

| Kiasi | Pamoja na VAT | Kiasi | Pamoja na VAT |
|---|---|---|---|
| 1,000 - 3,999 | 335 | 300,000 - 399,999 | 6,037 |
| 4,000 - 4,999 | 447 | 400,000 - 499,999 | 6,596 |
| 5,000 - 9,999 | 615 | 500,000 - 599,999 | 7,043 |
| 10,000 - 19,999 | 1,230 | 600,000 -999,999 | 7,266 |
| 20,000 - 39,999 | 1,453 | 1,000,000 - 1,999,999 | 7,658 |
| 40,000 - 49,999 | 1,677 | 2,000,000 - 2,999,999 | 8,050 |
| 50,000 - 99,999 | 2,012 | 3,000,000 - 3,999,999 | 8,385 |
| 100,000 - 199,999 | 3,745 | 4,000,000 - 4,999,999 | 8,944 |
| 200,000 - 299,999 | 4,975 | 5,000,000 - 6,000,000 | 9,503 |

| Jina na Cheo | Signature | Date |
|---|---|---|
| Mwijage B Bishota (Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu) | Signed | 20 Januari 2022 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha ) | Signed | 20 Januari 2022 |
| Modest Kissima (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | Signed | 20 Januari 2022 |

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### HAALAND KUISIKILIZIA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland, 21, anataka kusubiri kuchukua uamuzi juu ya hali yake ya baadaye ili kuona iwapo Barcelona wataweza kumsajili. ***(Star)***

#### PHILLIPS ATENGEWA DAU

KLABU ya West Ham United imepanga dau la pauni milioni 50 kwa ajili ya kumsajili kiungo, wa Leeds United na England, Kelvin Phillips, 26. ***(Sun on Sunday)***

#### STERLING ASUBIRIWA KUAMUA

MANCHESTER City watasikiliza ofa kwa kusitasita kwa ajili ya mshambuliaji wa England, Raheem Sterling, 27, msimu huu kama watashindwa kukubaliana naye juu ya kurefushwa kwa mkataba wa mchezaji huyo ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika msimu ujao. ***(Star)***

#### AUBAMEYANG SAFI BARCA

BARCELONA wamefikia makubaliano na mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 32, kumsajili kwa mkopo kutoka Arsenal, lakini watahitaji kumuachia Ousmane Dembele ili kukamilisha taratibu za uhamisho. ***(Gerard Romero, via Metro)***

#### DE BEEK AGOMBEWA

KLABU ya Everton imejiunga na Crystal Palace katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek, 24, kutoka Manchester United. ***(Athletic)***

#### UNITED KUMWACHIA DE BEEK

KLABU ya Manchester United itamwachia Donnyc Van de Beek aondoke ili mradi matakwa yao ya mkataba yatimizwe. ***(90 Min)***

#### CAVANI KUPISHANA ALVAREZ

KLABU ya River Plate inapanga kumbadilisha Muargentina, Julian Alvarez, 21, ambaye analengwa na Manchester City na mshambuliaji wa Manchester United, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34. ***(Mirror)***

#### SPURS OFA KWA BENTANCUR

TOTTENHAM Hotspur wamempa ofa ya euro milioni 30 na marupurupu ya ziada kiungo wa kati wa Juventus, Rodrigo Bentancur ambaye amehusishwa na Aston Villa. ***(Gianluca di Marzio, via 90 Min)***

#### MADRID KWA SALIBA ARSENAL

MLINZI wa Arsenal, William Saliba, 20, ambaye anacheza kwa mkataba wa mkopo katika klabu ya Marseille yuko kwenye orodha ya wachezaji wanaolengwa na Real Madrid msimu huu. ***(Sport, via Metro)***

#### MORATA HAENDI BARCA

KLABU ya Atletico Madrid hawatamwachia mshambuliaji wa Hispania, Alvaro Morata, 29, ambaye anachezea Juventus kwa mkopo ili ajiunge na Barcelona. Arsenal, Newcastle United na Tottenham Hotspur wanania na mchezaji huyo. ***(Sport, via Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GIROUD AFUNGUKA KUPATA DARASA KWA IBRAHIMOVIC

Ni fursa nzuri kuwa naye, najifunza vitu zaidi, yeye ni mfano kwa washambuliaji wengi na...

**MILAN,** Italia

OLIVIER Giroud anafurahia "mashindano yenye afya" na Zlatan Ibrahimovic na amesema mchezaji mwenzake huyo wa AC Milan anamsukuma kuwa bora.

**Ibrahimovic amefanya makubwa katika kipindi chake cha pili akiwa na Milan tangu arejee katika klabu hiyo Januari 2020, na kufunga mabao 36 katika mechi 66 kwenye michuano yote.**

Ameanza mara 12 pekee msimu huu, lakini amethibitisha thamani yake tena kwa kuzifumania nyavu mara nane.

Kwa bao lake dhidi ya Udinese Desemba, Ibrahimovic alijiunga na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo kuwa miongoni mwa wachezaji waliofunga mabao 300 katika Ligi Kuu tano bora za Ulaya.

Huku kukiwa na ripoti nchini Italia kwamba Milan iko tayari kumpa mkataba mwingine hadi mwishoni mwa msimu ujao, Giroud anashukuru kuwa ana nafasi ya kujifunza kutoka kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 40.

"Kucheza naye ni jambo ambalo naona kama changamoto, jambo ambalo linanisukuma kila siku," alisema Giroud akiiambia Colinterview - Oh my Goal YouTube channel.

"Ni fursa nzuri kuwa naye, najifunza vitu zaidi.

"Yeye ni mfano kwa washambuliaji wengi na nilipokuwa mdogo nilimpenda, tabia yake inanifanya nijifunze mambo mengi sana kila siku. "Ni ushindani mzuri kati yetu."

Giroud alitua pale San Siro akitokea Chelsea Julai mwaka jana akiwa na mabao sita na asisti moja katika mechi 20 za kwanza, 11 kati ya hizo akianza.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
PARIS ST GERMAIN
VERSUS
NICE
1 | 1.52
X | 4.19
2 | 5.59

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# FAMILIA YAMTAKA BALE AONDOKE REAL

**MADRID,** Hispania

GARETH Bale anatarajiwa kuondoka Real Madrid mwishoni mwa msimu huu, lakini familia na marafiki ndio chanzo cha kumtaka afanye hivyo.

Akiwa ametumia msimu uliopita kwa mkopo kule Tottenham Hotspur, Bale amerejea Madrid kwa mwaka wa mwisho wa mkataba wake, ambao unamalizika Juni, mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ataondoka kama mchezaji huru, hivyo kumaliza muda wake wa miaka tisa baada ya kujiunga na 'Los Blancos' kwa mara ya kwanza.

Majeruhi yamemfanya Bale kuwa nje ya uwanja kwa muda mwingi wa msimu na hajacheza tangu Agosti kwa sababu ya matatizo ya goti. Lakini alirejea kwenye benchi wakati Real ikitoka sare na Elche kwenye mchezo wa La-Liga wikendi iliyopita.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca, heshima ya Bale pale Madrid imerejeshwa baada ya kuteuliwa tena kwa Carlo Ancelotti, ambaye chini yake alishinda taji lake la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2014.



# Cameroon, Burkina Faso nusu fainali

**YAOUNDE,** Cameroon

KARL Toko Ekambi amefunga mabao mawili kipindi cha pili na kuwawezesha wenyeji Cameroon kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Gambia na kutinga nusu fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), juzi usiku, huku Burkina Faso ikiitoa Tunisia.

Ekambi aliifungia nchi yake bao la kuongoza dakika ya 50, akiunganisha krosi ya Collins Fai na dakika saba baadaye akafunga la pili akitumia uzembe wa Martin Hongla.

Cameroon itacheza na Misri au Morocco katika nusu fainali Alhamisi, na fainali itapigwa Jumapili ijayo.

Gambia ilikuwa inashiriki michuano hiyo kwa mara ya kwanza na kuzishinda Mauritania na Tunisia katika hatua ya makundi na kutinga mtoano, kabla ya kuiondoa Guinea katika hatua ya 16 bora.

Lakini, mbele ya umati wa watu wa nyumbani wenye shauku katika Uwanja wa Japoma pale Douala, Gambia walizidiwa katika kila idara.

Katika mechi ya pili ya robo fainali hiyo, kinda Dango Ouattara alifunga bao pekee na kutolewa nje kwa kadi nyekundu wakati Burkina Faso ikiishangaza Tunisia kwa kuwatungua 1-0 na kutinga nusu fainali.

Ouattara mwenye umri wa miaka 19, alikimbilia mpira uliopigwa na Blati Toure na kuwachenga mabeki wawili na kupiga shuti kali lililojaa wavuni. Lakini alitolewa kwa kadi nyekundu dakika ya 82 kwa kumpiga kiwiko, Ali Maaloul.

Burkina Faso sasa watakutana na mshindi wa mchezo wa jana Jumapili kati ya Senegal na Equatorial Guinea.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# SPORTPESA YAZINDUA MULTIBET BONASI YA KIBABE

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Michezo na Burudani ya SportPesa imezindua huduma mpya ya Multibet Bonasi kwa wachezaji wake wote nchini.

Bidhaa hiyo ni ya kwanza na ya kipekee kwa wachezaji wao kutokana na kiwango cha asilimia ambacho mteja atakuwa anakipata baada ya kuweka ubashiri wake kuanzia mechi tatu.

Akizungumzia bonasi hiyo mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Utalawa na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas (pichani), alisema wameamua kufungua mwaka kwa kishindo, kwa kuwaongezea wateja wao kiwango cha asilimia za mapato kwenye 'odds', katika mechi watakazokuwa wanachagua na kuweka bashiri wakati wa kupanga mikeka yao.

"Wachezaji wetu watapata bonasi mpaka asilimia 85 ya kiasi ya kubet kulingana na idadi ya timu watakazochagua katika bashiri zao," alisema Tarimba.

Alisema wachezaji watakaoruhusiwa kushiriki fursa hii ni wale watakaokuwa wanabashiri na 'odds' zisizopungua 1.2 na timu za kuchagua zisizopungua tatu.

"Tunajua kuna wachezaji wetu wanaopenda kucheza mechi nyingi, hivyo basi huduma hii imelenga kuwaongezea chachu ya kucheza mechi nyingi zadi kadiri wawezavyo ili wapate zaidi kama asilimia zitakavyojiongeza," alisema.



Alisema bidhaa hiyo ya Multibet Bonus, itakuwa inapatikana kupitia Sportpesa App yao, inayopatikana kwa watumiaji wa simu janja na pia kupitia website ya www.sportpesa.co.tz, kwa wanaotumia kompyuta mpakato pekee na kwamba huduma hiyo ya Multibet Bonasi, ni moja ya bidhaa bunifu kutoka kwao ambayo itakuwa inapatikana kwenye mechi za kila siku.

"Haya ni maboresho ambayo kampuni imeamua kuyaongeza katika kukupa wewe mteja ama mchezaji fursa ya kupata zaidi katika kila ubashiri utakaokuwa unaouweka."

Sambamba na bidhaa hii, SportPesa inajitahidi kuboresha huduma zake zote ili ziweze kukidhi malengo na matakwa ya wachezaji wake, pamoja na soko kwa ujumla, kwa kiwango.

# *Washindi Kilimanjaro Marathon kuzawadiwa viwanja*

Na Mwandishi Wetu

WAANDAAJI wa Kilimanjaro Premium Lager Marathon, wametangaza mdhamini mpya wa mbio hizo, Surveyed Plots Company (SPC) Ltd ya jijini Dar es Salaam ambayo itatoa zawadi ya viwanja kwa Mtanzania wa kwanza wa kiume na wa kike katika mbio za Km. 42 za mwaka huu.

Mkuu wa Uendeshaji wa kampuni ya SPC, Kenny Rodgers, ndiye aliyeweka wazi ahadi hiyo mwishoni mwa wiki huku akieleza kuwa wanajivunia kuwa sehemu ya mashindano makubwa ya Kilimanjaro Marathon 2022

"Gharama zote za kusajili viwanja hivyo kwa majina ya washindi zitagharamiwa na Kampuni ya SPC Ltd. Tutafanya utaratibu wa kuwamilikisha viwanja hivyo kwa majina yao na kuwapa nyaraka zote," alisema.

"Hili ni tukio kubwa na ni nafasi nzuri kwetu kujitangaza kwani haya ni mashindano makubwa ya riadha katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki na hasa ikizingatiwa kuwa mashindano hayo yanaadhimisha miaka 20," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa Watanzania kujifua na kujiandaa vizuri kwa mbio hizo za Km. 42 ili wajishindie viwanja hivyo.

"Tunaamini ushindani utakuwa mkubwa, kwa hiyo watakaojiandaa vizuri wana nafasi kubwa sana ya kushinda mwisho wa siku," alisema.

Wadhamini wa mbio za Kilimanjaro Marathon 2022 ni Kilimanjaro Premium Lager (Mdhamini Mkuu) Tigo (Km. 21 na Grand Malt (Km. 5).

Wadhamini wa meza za maji ni pamoja na Absa Tanzania, Unilever Tanzania, TPC Sugar, Simba Cement na Kilimanjaro Water. Wasambazaji rasmi ni Garda World Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel, CMC Automobiles na Surveyed Plots Company Ltd (SPC) na Bodi ya Utalii (TTB).

Katika hatua nyingine, kwa mujibu wa waandaaji wa Kilimanjaro Marathon, kwa mara ya kwanza kutakuwako na maonyesho yanayojulikana kama Kili Expo (The People's Expo) ambapo wadhamini na wadau wengine wa mbio hizo watapata fursa ya siku tatu za kuonyesha bidhaa na huduma wanazotoa, maonyesho ambayo yanatarajiwa kufanyika kati ya Februari 24-26, mwaka katika viwanja vya MoCU.

Mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon, zinatarajiwa kufanyika Jumapili ya Februari 27, mwaka huu, katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), ambapo zimeandaliwa na Taasisi ya Kilimanjaro Company Limited na kuratibiwa na wadau wa hapa nchini Kampuni ya Executive Solutions Limited.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 31/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5006 | SP. Braga U23 vs Rio Ave U23 | 1.48 | 3.95 | 5.78 |
| 15:45 | 2518 | Laci vs Partizani Tirana | 2.23 | 2.85 | 3.33 |
| 15:45 | 5984 | Egnatia Rrogozhine vs Din. Tirana | 3.23 | 2.85 | 2.28 |
| 15:50 | 5861 | Al Jabalain vs Al Wehda | 2.56 | 2.85 | 2.80 |
| 16:00 | 5064 | Dire Dawa Kenema FC vs Mekelakeya | 2.70 | 2.79 | 2.70 |
| 16:00 | 5469 | APR FC vs Mukura | 1.33 | 4.51 | 8.07 |
| 16:30 | 1260 | AL Wakrah vs Al Sadd SC | 8.49 | 5.79 | 1.24 |
| 17:00 | 5971 | Northeast United FC vs Hyderabad FC | 4.83 | 4.06 | 1.55 |
| 18:00 | 4879 | AL Sahel SC vs Najran SC | 2.39 | 2.84 | 3.03 |
| 18:30 | 4704 | Panathinaikos U19 vs Asteras Tripolis U19 | 1.70 | 3.71 | 4.15 |
| 18:45 | 3076 | Skenderbeu vs Teuta Durres | 3.27 | 2.94 | 2.20 |
| 19:00 | 4488 | Welayta Dicha FC vs Arba Minch Kenema | 2.27 | 2.85 | 3.24 |
| 19:45 | 3794 | AL Draih vs AL Adalh | 2.65 | 2.89 | 2.65 |
| 20:00 | 1172 | Hapoel Afula vs Hapoel Rishon Lezion | 2.98 | 2.83 | 2.63 |
| 20:00 | 1511 | Sectzya Nes Ziona vs Hapoel Ramat Gan | 2.12 | 3.11 | 3.60 |
| 20:00 | 1568 | Aris Limassol vs AEL Limassol | 2.16 | 3.22 | 3.37 |
| 20:00 | 2295 | Casa Pia Atletico vs Penafiel | 1.82 | 3.36 | 4.19 |
| 20:00 | 3355 | SC Kfar Qasem vs Ironi Hasharon | 1.81 | 3.42 | 4.46 |
| 20:30 | 2298 | AS Tel Aviv University W vs Hapoel Marmorek Rehovot W | 1.30 | 4.70 | 8.64 |
| 21:00 | 1534 | CFR Cluj vs Botosani | 1.61 | 3.61 | 5.47 |
| 21:00 | 2926 | Ironi Kiryat Shmona vs Bnei Sakhnin | 2.02 | 3.17 | 3.46 |
| 21:00 | 3570 | Atlas W vs Puebla FC W | 1.20 | 6.18 | 9.66 |
| 21:00 | 4750 | Eintracht Braunschweig vs Verl | 1.79 | 3.67 | 4.01 |
| 21:30 | 1696 | Waasland Beveren U21 vs Jeugd Rfc Seraing United U21 | 1.77 | 3.81 | 3.66 |
| 21:30 | 2451 | Zulte Waregem U21 vs Standard Liege U21 | 4.62 | 4.33 | 1.53 |
| 21:30 | 3237 | Antwerp U21 vs Mechelen U21 | 1.70 | 4.20 | 4.30 |
| 21:30 | 3476 | Club Nxt vs Charleroi U21 | 1.47 | 4.43 | 5.21 |
| 21:30 | 3782 | Anderlecht U21 vs St Truiden U21 | 1.17 | 6.54 | 10.58 |
| 21:30 | 5494 | Kortrijk U21 vs AS Eupen U21 | 6.20 | 5.20 | 1.42 |
| 21:30 | 5918 | Cercle Brugge U21 vs KRC Genk U21 | 6.20 | 4.84 | 1.37 |
| 21:30 | 5977 | KAA Gent U21 vs OH Leuven U21 | 1.60 | 4.15 | 4.25 |
| 22:00 | 1289 | Westerlo U21 vs Excelsior Virton U21 | 1.89 | 3.76 | 3.28 |
| 22:00 | 2771 | Vasas SC vs Diosgyori Vtk | 1.93 | 3.55 | 3.85 |
| 22:00 | 3776 | GD Estoril vs Pacos Ferreira | 2.15 | 3.11 | 3.46 |
| 22:00 | 3985 | Lierse SK vs Union Saint Gilloise U21 | 3.28 | 3.66 | 1.92 |
| 22:00 | 4380 | Lommel U21 vs RWD Molenbeek U21 | 3.86 | 4.15 | 1.67 |
| 22:00 | 4640 | Orsomarso vs Deportes Quindio | 4.53 | 3.42 | 1.70 |
| 22:00 | 4797 | Kmsk Deinze U21 vs Mouscron U21 | 3.56 | 3.75 | 1.81 |
| 22:00 | 5661 | Beerschot Wilrijk U21 vs Oostende U21 | 2.52 | 3.63 | 2.34 |
| 22:45 | 3664 | Portsmouth vs Charlton | 2.08 | 3.24 | 3.44 |
| 23:00 | 4759 | Juve Stabia vs Foggia | 2.42 | 3.02 | 3.07 |
| 23:00 | 5967 | UD Ibiza Eivissa vs Zaragoza | 2.13 | 3.09 | 3.48 |
| 23:15 | 2135 | Paris St Germain vs Nice | 1.52 | 4.19 | 5.59 |

JUMANNE - 01/02/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:10 | 2256 | Japan vs Saudi Arabia | 1.49 | 3.66 | 6.36 |
| 15:00 | 1407 | Lebanon vs Iraq | 2.54 | 2.83 | 2.83 |
| 15:00 | 3597 | Vietnam vs China | 3.37 | 3.32 | 1.99 |
| 17:30 | 1832 | Iran vs United Arab Emirates | 1.60 | 3.56 | 5.19 |
| 23:00 | 2471 | Bolivia vs Chile | 2.76 | 3.11 | 2.66 |
| 23:15 | 5446 | Santa Clara vs Boavista | 2.22 | 3.11 | 3.30 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatatu Januari 31, 2022

Nipashe




Giroud afunguka kupata darasa kwa Ibrahimovic UKURASA 21

HATUPOI...!



Wachezaji wa Yanga wakishangilia moja ya ushindi walioupata kwenye Ligi Kuu msimu huu. **PICHA: MAKTABA**

## Wanasoka watano matajiri zaidi 2022




**LONDON,** Uingereza

SOKA ndio mchezo maarufu zaidi duniani. Hakika ni mchezo...

HABARI UK. 11

## Cameroon, Burkina Faso nusu fainali Afcon

**YAOUNDE,** Cameroon

KARL Toko Ekambi amefunga mabao mawili kipindi cha pili na kuwawezesha...




HABARI UK. 22

# Yanga: Moto huu hauzimiki

## ●●● Mayele azidi kuipa jeuri ya makombe, kipa atamani kiwango cha Mkongomani huyo Stars...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema baada ya kukosa Kombe la Mapinduzi, inataka kutwaa makombe yote mawili yaliyobaki ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA na moto ambao wameuwasha hakuna wa kuuzima.

**Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 10 zaidi ya Mabingwa Watetezi, Simba wenye alama 25 katika nafasi ya pili ya ligi hiyo, juzi iliitoa Mbao FC katika mchezo wa raundi ya 32 ya Kombe la FA uliopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza baada ya kushinda 1-0, shukrani kwa Fiston Mayele aliyefunga bao hilo pekee.**

Na kutokana na mwenendo mzuri kwenye Ligi Kuu na Kombe la FA, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema kwa bahati mbaya sana wamelikosa Kombe la Mapinduzi, lakini kwa sasa lengo lao ni kuchukua makombe yote mawili makubwa yaliyobaki na uhakika huo wanao kwa sababu wana kikosi cha wachezaji imara, benchi la ufundi lililo bora na viongozi thabiti.

"Mchezo ulikuwa mzuri na watu wamefurahi sana, timu zote zimecheza mpira mzuri, ingawa Yanga tumecheza vizuri zaidi. Lengo letu mwanzo lilikuwa kuchukua makombe yote matatu, lakini moja tumeliachia, haya mawili tutahakikisha tunachukua na nina uhakika kwa hilo kwa sababu msimu huu tuna kikosi imara, benchi la ufundi bora na viongozi thabiti, tunaamini moto huu hakuna wa kuuzima," alisema Bumbuli ambaye timu yake sasa imeingia hatua ya 16 bora.

Hata hivyo, amesema ameshangazwa na ubora wa timu ya Mbao FC kwenye mechi hiyo, akiongeza kuwa endapo wataendelea kucheza hivyo kama walivyocheza kwenye mechi hiyo, basi ana uhakika watatoka kwenye Ligi Daraja la Kwanza na kutinga ngazi ya Championship.

"Mbao wako vizuri, kama wanacheza hivi kwenye Ligi Daraja la Kwanza, wanaweza kurudi Championship, lakini kama wamecheza hivi kwa sababu wamecheza na Yanga kama ambavyo wanafanya Coastal Union ambao wao kazi yao ni kuikamia Yanga, basi watakuwa kama wao tu, wakimaliza kucheza na sisi mechi zinazofuata wanafungwa tu," alisema.

Wakati huo huo, kikosi cha Yanga kimerejea Dar es Salaam kuendelea na maandalizi ya mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Mbeya City, inayotarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Jumamosi wiki hii.

Katika hatua nyingine, Kipa wa Mbao FC, Wandwi Jackson amekiri kuwa straika wa Yanga, Mayele ni hatari, akitamani Watanzania kuwa na mchezaji kama yeye ili kuisaidia timu ya Taifa, Taifa Stars.

Wandwi amesema kuwa kwa dakika zote 90 alizokuwa golini mtu ambaye alikuwa hatari zaidi ni Mayele kutokana na mikimbio yake na kujua kukaa kwenye maeneo ambayo ni hatari kama mabeki hawakuwa makini.

"Huyu jamaa yupo vizuri chini, yupo vizuri juu, wakati wenzake wana mpira, yeye anajua wapi aende kukaa ili iwe rahisi kwake kucheza. Halikimbii goli, muda wote wenzake wakitaka kupiga krosi yupo golini, ndiyo maana nilikuwa nawapigia kelele sana mabeki wangu na kuwakumbusha wamchunge sana kwa sababu wachezaji wote wa Yanga ndiyo wanamtegemea yeye na kumpigia yeye tu krosi, na jinsi anavyopambana kuipata mipira.

"Niliwaambia mkizembea wakati wowote anaweza kutudhuru na kweli, mpira huo huo wa krosi ndiyo uliotudhuru kwa kosa moja tu," alisema kipa huyo akiongea kwa tabu kutokana na kukauka sauti kwa ajili ya kuwapigia kelele mabeki wake.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >